# USAWIRI WA WAHUSIKA MAKAHABA KATIKA RIWAYA ZA SAID AHMED MOHAMMED

NA

MUINDI AUGUSTINE

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya 'Masters of Arts' katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

1990.

Augustine, Muindi
*Usawini wa wahusika makahaba katika*
91/197914

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya digrii katika chuo kikuu kingine.

Augustine Muindi
(MTAHINIWA)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yangu kama msimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu.

P.J.M. Mugambi
(MHADHIRI: IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA)

K.U

# YALIYOMO

| | | Ukurasa |
|---|---|---|
| Yaliyomo | | i |
| Shukrani | | iii |
| Muhtasari | | iv |
| **SURA YA KWANZA** | | |
| 1.0. | Utangulizi wa Utafiti | 1 |
| 1.1. | Mada ya Utafiti | 1 |
| 1.2. | Madhumuni ya Utafiti | 5 |
| 1.3. | Sababu za kuchagua mada hii | 8 |
| 1.4. | Upeo wa Utafiti | 9 |
| 1.5. | Yaliyoandikwa kuhusu mada hii | 10 |
| 1.6. | Msingi wa nadharia ya Utafiti | 15 |
| 1.7. | Njia za Utafiti | 18 |
| **SURA YA PILI** | | |
| 2.0. | Dhana na nadharia za ukahaba | 20 |
| 2.1. | Dhana ya ukahaba | 20 |
| 2.2.0. | Nadharia za ukahaba | 28 |
| 2.2.1. | Nadharia ya upembuzi wa nafsi | 28 |
| 2.2.2. | Nadharia ya utekelezi | 33 |
| 2.2.3. | Nadharia ya Ki-Marx | 37 |

Ukurasa

SURA YA TATU

3.0. Wahusika makahaba na sababu zinazowavuta ____ 44

3.1.1. Wahusika wanaochuma kwa kuuza miili yao ____ 46

3.1.2. Wahusika wanaohusiana kwa misingi ya kifedha au faida ____ 68

SURA YA NNE

4.0. Jinsi mwandishi anawaondosha wahusika wake kutoka kwa maisha ya ukahaba 88

4.1. Matumizi ya kifo katika fasihi ____ 91

4.2. Kuhamia mazingira ya mashambani ____ 99

4.3. Taasisi ya ndoa ____ 122

SURA YA TANO

5.1. Hitimisho ____ 119

Marejeleo ____ 127

# SHUKRANI

Natoa shukrani nyingi kwa msimamizi wa kazi hii Bwana Peter Mugambi kwa kuniongoza na kunipa mashauri yaliyonifaa sana.

Pia, nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kwa kunihimiza na kunitia shime katika masomo yangu.

Kufaulu kwangu kumetokana na ushirikiano wa wanafunzi wenzangu. Wote nawashukuru.

Aidha, nawashukuru wazazi wangu wapenzi. Walinifunza subira na unyenyekevu. Walijinyima mambo mengi ya lazima ili nipate elimu yangu. Walinipa nguvu pale niliposinzia.

Masomo yangu ya shahada ya 'Masters of Arts' yamegharamiwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta. Natoa shukrani kwa chuo hicho na hasa kwa Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kwa kuniteua niendelee na masomo.

Mwisho, ahsante Mary Khaemba kwa kunipigia chapa kazi hii.

## MUHTASARI

Utafiti wetu unahusu suala la ukahaba katika riwaya nne za Said Ahmed Mohamed. Tunahakiki usawiri wa wahusika makahaba kwa madhumuni ya kubainisha sababu za kuwepo kwa ukahaba katika jamii. Aidha, tunatalii namna ambavyo mwandishi anawabadilisha wahusika wake kutoka kwa maisha ya ukahaba na kama mabadiliko hayo yanatoa suluhisho halisi kwa jamii ya makahaba.

Sura ya kwanza ni utangulizi wa utafiti. Hapa ndipo tunapojadili tasnifu kwa jumla, mada ya utafiti, madhumuni ya utafiti wetu, upeo wa utafiti wetu. Vile vile, tunajadili baadhi ya kazi nyingine zilizowahi kuandikwa na ambazo kwa namna fulani, zinahusiana na utafiti wetu. Aidha, tutasema machache kuhusu nadharia tunayotumia katika utafiti wetu. Kisha tutatazama sababu za kuchagua mada hii na njia tutakazofuata katika kutafiti juu ya mada yetu.

Katika sura ya pili na ambayo ndiyo nguzo ya utafiti, tunaelezea dhana na nadharia za ukahaba. Dhana na nadharia hizi zinatusaidia katika kubainisha vigezo mbalimbali vinavyotambulisha kahaba katika jamii.

Tunafikia upeo wa utafiti wetu katika sura ya tatu na nne. Katika sura ya tatu, tunanuia kubainisha sababu

mbalimbali ambazo zimewavuta baadhi ya wahusika katika maisha ya ukahaba. Sura ya nne, tunajadili namna ambavyo mwandishi anawaondoa wahusika wake kutoka kwa maisha hayo.

Sura ya tano ni ya hitimisho. Tunatoa muhtasari wa kazi tuliyoifanya. Kisha, tunatathmini kama tumefikia malengo ya utafiti wetu. Mwisho kabisa, tunatoa marejeleo ya utafiti wetu.

# SURA YA KWANZA

## 1.0. UTANGULIZI WA UTAFITI

## 1.1. MADA YA UTAFITI

Tasnifu hii inajadili usawiri wa wahusika makahaba katika riwaya nne za Said Ahmed Mohamed. Fikira za waandishi kuhusu jamii kwa jumla hujazwa kwa wahusika. Hivyo basi, hoja muhimu hapa ni kujaribu kuona kwa nini Said A. Mohamed amewasawiri baadhi ya wahusika wake kama makahaba. Aidha, tunahakiki jinsi uumbaji huu unavyolingana na uhalisia wa maisha.

Kulingana na maelezo yake Mbilinyi [1983:14], mwanamke alianza kuonekana kama suala la utafiti hapa Afrika Mashariki mwanzoni mwa miaka ya sitini. Huu ndio wakati ambapo mataifa mengi yalianza kujipatia uhuru. Serikali zilihamasishwa kutafiti kuhusu nyanja nne zinazohusiana na mwanamke. Utafiti ulihitajika kuhusu idadi kubwa ya wanawake waliokuwa wakijiingiza katika ukahaba, wasichana wengi wa shule kupata mimba, idadi kubwa ya wasichana kukimbilia mijini, kisha uasherati kuongezeka miongoni mwa wasichana na wanawake.

Kuhusu suala la ukahaba, kuna utafiti kidogo sana ambao umefanywa [Senkoro 1982:IX] na utafiti wa kindani unahitajika. Utafiti kuhusu mada hii unafaa ndipo tuweze kumulika na kuona ni kwa nini idadi ya makahaba inazidi kuongezeka mijini na vichochoroni. Utafiti wetu unashabihiana sana na nyanja ambazo Mbilinyi [1983] anazungumzia. Tunapozungumzia ukahaba, sharti tuone ni kwa namna gani unavyotumiwa kama suluhisho na wasichana wanaopata mimba wakiwa shuleni na kadhalika. Pia, lazima tuhusishe ukahaba na idadi kubwa ya wasichana na wavulana wanaokimbilia mjini kila siku. Licha ya hayo, ukahaba huenda sambamba na uasherati.

Kuna uhusiano mkubwa kati ya ukahaba na unyonge, Bakwesegha [1982:11]. Unyonge kwa muktadha huu unamaanisha udhaifu wa kiuchumi pamoja na udhaifu wa nafsi. Aghalabu makahaba ni wahitaji; uhitaji wa kiuchumi na uhitaji wa kuridhisha nafsi yenye kiu ya 'mapenzi'. Wa aidha, kuna unyonge unaosababishwa na kufiwa au kutengwa na walezi. Hali hii mara nyingi husababisha malezi mabaya pamoja na madhara ya kiuchumi. Talaka na himila nje ya ndoa mara nyingi husababisha unyonge wa nafsi na kiuchumi. Kwa hivyo, utafiti wetu utamulika kuona vile unyonge umewalemaza wahusika wengi hadi kiwango cha ukahaba.

Suala la ukahaba lina uzito wake, maana ni suala linalostahili kuwekewa mipaka yake. Mwanamke ndiye kahaba peke yake au mwanamume ni kahaba pia. Kahaba [Winiston Dictionary, 1948] ni mwanamke au mwanaume anayeshiriki mambo ya uasherati kwa matumaini ya kupata pesa. Aidha, Kishtainy [1982:32], Dirasse [1978:15], Muga [1980:25] na Bakwesegha [1982:30] wanaeleza kuwa, kahaba ni mwanamke au mwanamme anayeshiriki mapenzi na watu wengi kwa matarajio ya pesa au zawadi na bila kuwa na mshikamano wa kihisia. Kwa muktadha huu, sharti tubainishe vigezo vinavyomtambulisha kahaba.

Kwa mkururo huu wa maelezo, kahaba awe wa kiume au wa kike hubadilisha mwili wake na kitu kingine. Kwa mtazamo wa elimu-jamii, ukahaba ni kazi kama kazi nyingine yoyote na unatekeleza jukumu muhimu la kiuchumi katika jamii. Tukiutazama ukahaba kwa upande wa elimu-nafsi, tutaona kuwa washiriki hujiingiza katika tabia hii kwa madhumuni ya kuridhisha nafsi zenye kiu ya 'mapenzi'. Kwa hivyo, wote wawili, mwanamke na mwanamme ni nguzo katika kuendeleza taasisi ya ukahaba. Wote hunufaika kwa viwango tofauti; kiuchumi au kuridhisha nafsi.

Kwa kushikilia uzi ule ule hatuna budi kuwawekea makahaba mipaka kama wanavyosawiriwa katika riwaya za

Said Ahmed Mohamed. Kuna wale makahaba tunaowapata katika danguro wakiuza miili yao kwa minajili ya kujipatia pesa ili kujiendeleza. Hili ndilo tabaka duni zaidi kwa upande wa makahaba.

Kuna wale wanaume na wanawake wanaowajibika kusalimisha miili yao kwa madhumuni ya kufaidika. Wanaohusika katika kundi hili hawapatikani katika danguro, lakini wanapatikana katika nyanja tofauti za kimaisha. Katika kundi hili, tunahusisha wasichana wanaokubali kuepeana miili yao ndipo waajiriwe kazi, wapandishwe cheo au kuongezwa mshahara. Hiki ni kitendo cha ukahaba maana wanaoshiriki hubadilisha miili na kazi au mshahara.

Hatuna budi kujadili namna 'Mashuga-dadi' na 'Mashuga-mami' wanavyochangia ukahaba. Kuna wale wanawake au wanaume wanaopeana miili yao bila kutarajia pesa. Wa aidha, wenyewe wanawapatia vijana wabichi pesa. Kwa muktadha huu, hawa vijana hujiuza kwa hawa 'akina mama' na 'akina baba' ndipo wapate pesa au faida nyingine. Aghalabu, 'Mashuga-dadi' na 'Mashuga-mami' huwakimbiza vipusa na mabarubaru kwa madhumuni ya kutaka kuridhisha nafsi zao zenye kiu ya mapenzi. Kwa mujibu wa uhitaji wa

kiuchumi, hawa vipusa na mabarubaru huwajibika kuuza miili yao.

Uhakiki wetu unahusu viwango hivi tofauti vya makahaba. Tunanuia kuona ni kwa nini Said A. Mohamed amewasawiri hivyo katika riwaya zake. Wanasaidia kusafirisha maudhui yepi mengine.

Tasnifu hii inajishughulisha na ukamilifu wa jamii. Tumetumia neno ukamilifu kwa maana kwamba tunautuzama ukahaba kama tabia inayoendelezwa na mwanamke na mwanamume. Wote wawili ni washiriki na ni lazima utafiti uhusishe wote wawili.

## 1.2. MADHUMUNI YA UTAFITI

Katika tasnifu hii, kuna mambo kadha wa kadha ambayo tunataka kubainisha. Madhumuni ya kwanza ya hii tasnifu ni kujaribu kubainisha hoja mbalimbali zinazosababisha ukahaba. Baadhi ya wasichana na wavulana wamejikuta mijini wakiuza miili yao kutokana na uhitaji wa kiuchumi. Kwao, ukahaba ni kama kazi nyingine yoyote ya kuendeleza maisha.
Idadi kubwa wameonewa kwa njia moja ama nyingine, Chambilecho Kishtainy (1982:9):-

> "Idadi kubwa ya wanawake tunaowapata katika danguro wanatokana na kundi la wanyonge... Wasichana wanaofanya kazi za nyumbani, wanaotongozwa, kutiwa mimba na waajiri wao na kufukuzwa..." (tafsiri yetu).

Hata hivyo, si wote ambao wanajiingiza katika ukahaba kwa sababu za kiuchumi. Kuna wengine ambao wameongozwa na sababu za kisaikolojia, uzembe na kadhalika. Sababu hizi tutaziainisha katika tasnifu hii.

Lengo lingine ambalo tunanuia kufikia katika utafiti huu ni kutathmini hisia za kijamii kuhusu ukahaba. Tasnifu hii itachangia kuelewa kama makahaba wenyewe wanaufurahia ukahaba au wanahisi vipi. Isitoshe, tasnifu hii itapima hisia za jamii kuhusu ukahaba. Jamii ina utazama ukahaba vipi. Ukahaba ni uhuni, ukahaba ni kazi ya kujivunia au ukahaba ni kazi kama kazi nyingine yoyote. Malengo haya tutayafikia kwa kuhakiki hisia za wahusika, huku tukijua kwamba mwandishi ni mwakilishi na domo la jamii yake.

Madhumuni mengine ya hii tasnifu ni kujaribu kuona namna mwandishi anavyowaondosha wahusika wake kutoka katika maisha ya ukahaba. Swala hapa ni vipi Said A. Mohamed anawabadilisha wahusika wake makahaba na kama mabadiliko hayo yanatoa suluhisho halisi ya

ukahaba. Kwa kutaja tu, mwandishi amewarudisha baadhi ya wahusika wake makahaba mashambani, wengine amewaingiza katika taasisi ya ndoa, na upeo unafikia pale wengine wanakata tamaa na kujiua. Kwa hivyo, sharti tujishughulishe na matumizi ya kifo na ndoa katika fasihi, haswa kuhusiana na ukahaba.

Hatuna budi pia kutambulisha uhusiano uliopo kati ya ukahaba na maisha ya mjini. Uhakika ni kwamba, waandishi wengi wamewasawiri wanawake wa mjini kama makahaba au wenye maadili potovu ukilinganisha na wenzao wa huko mashambani. Tunajaribu kuangalia namna mazingira ya mjini yanavyochangia ukahaba tukilinganisha na yale ya mashambani. Kupitia kazi mbalimbali za fasihi, tumeona jinsi wanawake wanapochoshwa na maisha ya mashambani hukimbilia katika miji na kujiingiza katika ulevi na ukahaba. Utafiti wetu unalenga kutambulisha vipengee vinavyowabadilisha wasichana wengi mijini na hatimaye kuingilia ukahaba.

Tasnifu yetu ina madhumuni ya kuonyesha nafasi na dhima inayotekelezwa na wahusika makahaba katika riwaya za Said A. Mohamed. Mhusika yeyote anayejitokeza katika kazi ya fasihi sharti awe na jukumu na nafasi anayotekeleza. Tunanakidi usawiri wa wahusika makahaba kwa madhumuni ya kutathimini nafasi yao katika kuchangia

dhamira kuu.

## 1.3. SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Tumeamua kushughulikia usawiri wa wahusika makahaba kwa sababu kadhaa. Wahusika makahaba hutumulikia kuona ukandamizaji katika jamii. Fasihi zinazoonyesha ukandamizaji katika jamii ni muhimu sana maana zinatuelekeza kuelewa hali zetu pamoja na hali ya ulimwengu unaotuzunguka. Ukahaba ni hoja tunayoshuhudia katika jamii zetu. Tena, idadi ya makahaba inazidi kuongezeka. Hivyo basi, hii ni hoja ambayo haistahili kupuuza bali inastahili kufanyiwa utafiti kwa undani.

Tumehamasishwa kutafiti kuhusu usawiri wa wahusika makahaba kwa sababu usawiri huu hujumuisha maudhui ndani ya maudhui. Tunachojaribu kusema hapa ni kwamba uhakiki wa wahusika makahaba unaweza kutuongoza kuelewa maudhui mengine kama vile ufisadi katika baadhi ya viongozi, unyanyasaji wa wanawake, ubinafsi katika jamii na kadhalika.

Isitoshe, tumeamua kushughulika wahusika makahaba kwa kurejelea riwaya za Said A. Mohamed.

maana riwaya zake zinachambua kwa undani jamii zenye madhila na mateso kwa wanyonge na Kibri kwa watukufu, Mohamed (1980:XVIII). Zaidi ya hayo, riwaya zake ni mizani au kipimo cha kukadiria jinsi maisha ya jamii nyingi ziishizo ulimwengu wa tatu yalivyo, Kazungu (1984:IX). Hivyo basi, uhakiki wa usawiri wa wahusika makahaba utatufanya tuwaze juu ya maisha yetu kama watu binafsi na vile vile kama watu miongoni mwa jamii. Uhakiki huu utatufanya tujipeleleze, tujielewe, tujikanye na kujirekebishe.

## 1.4. UPEO WA UTAFITI.

Tasnifu yetu inahusu uhakiki wa usawiri wa wahusika makahaba. Tunachunguza usawiri huu kama unavyojitokeza katika riwaya nne za Said A. Mohamed zifuatazo:-

- Asali Chungu (Shungwaya Publishers, Ltd., Nairobi, 1977).
- Utengano (Longman, Nairobi, 1980).
- Dunia Mti Mkavu (Longman, Nairobi, 1980).
- Kiza Katika Nuru (Oxford University Press, Nairobi, 1988).

Said A. Mohamed ameandika kazi mbili za ushairi tuzijuazo. Hizi ni:-

Sikate Tamaa (Longman, Nairobi, 1980).

Kina Cha Maisha (Longman, Nairobi, 1984).

Pia, ameandika tamthilia moja, nayo ni:-

Pungwa (Longman, Nairobi, 1988).

Pia, ana mikusanyiko nyingi ya fasihi simulizi kama vile, Vito vya Hekima, Simo na Maneno ya Mshangao (Longman, Nairobi, 1974) na Simo, milio na Tashbihi (Longman, Nairobi, 1981).

Hatutajishughulisha na kazi hizi za ushairi, tamthilia na fasihi simulizi isipokuwa tu pale zinapoyataja maudhui ya ukahaba ili kuthibitisha na kutilia nguvu utafiti wetu. Utafiti wetu unahusu uhakiki wa wahusika wanaosawiriwa kama makahaba. Tutawajadili wahusika hawa huku tukibainisha sababu zinazowavuta katika ukahaba pamoja na namna mwandishi anavyojaribu kuwaondoa katika haya maisha ya ukahaba.

## 1.5. YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII

Miongoni mwa kazi ambazo zimeandikwa kuhusiana na hii mada ya ukahaba ni yake

Senkoro (1982). Senkoro ametafiti kuhusu maudhui ya ukahaba katika fasihi ya Kiafrika. Katika kazi yake, amerejelea vitabu vya fasihi vilivyoandikwa kwa kiingereza, Kiswahili na Kifaransa. Mtazamo wa Senkoro umeegemea zaidi upande wa waandishi ambao wameshughulikia mada hii. Kuna wale waandishi ambao wanamsawiri kahaba kama kiumbe potovu ambaye hana matumaini ya kujiondoa katika haya maisha. Amewataja waandishi kama vile Mailu (1973), Mohamed (1972), Sadji (1958). Senkoro anawashtumu waandishi hawa kwa kutojishughulisha kwa undani na kuelewa sababu zinazowaingiza wasichana wengi katika ukahaba. Sehemu yake ya pili imeonyesha jinsi ukahaba unavyotumika katika kazi ya fasihi kushtumu ukandamizaji wa tabaka duni. Senkoro anamtazama kahaba kama mwakilishi wa tabaka duni. Ni kweli lakini si makahaba wote ambao ni duni kiuchumi. Kuna wengine ambao wamejiweza sana kiuchumi. Jambo la pili ambalo Senkoro hakugusia kwa undani ni sababu zinazowavutia wasichana na wavulana wengi katika ukahaba. Ameonyesha sababu za kiuchumi bila kugusia sababu za kisaikolojia na kisosholojia. Aidha, haonyeshi nafasi ya wanaume katika kuendeleza ukahaba.

Naye Kishtainy (1982) amefanya mengi kuhusu maudhui ya ukahaba. Ametaja asili ya ukahaba katika

fasihi. Pia, anataja jinsi makahaba walivyotumiwa katika mahekalu takatifu huko Ugiriki. Kishtainy anazungumzia ukahaba katika jamii ambazo zimeuhalalisha na ukahaba ni kazi ya kujivunia na yenye pato la juu kuliko kazi ya ofisini. Hivi ndivyo asemavyo:-

> "Wanawake wengi hujiingiza katika kazi ya ukahaba maana mapato yake ni mengi kuliko kazi ya ofisini... Hali ya kiuchumi ya kahaba ukilinganisha na dadake ambaye si kahaba daima huwa nzuri" (Tafsiri yetu) (uk. 42).

Hali hii ambayo Kishtainy anatusawiria ni tofauti na hali tunayoina katika kazi zake Said A. Mohamed. Makahaba wengi katika riwaya za Said A. Mohamed ni duni na wanafanya kazi ya kijungu-jiko. Kazi yao si ya kujivunia. Kazi yake na yetu haiwezi kuwekwa mkabala mmoja maana zinahusiana na jamii mbili tofauti sana.

Kazi nyingine imefanywa na Strobel (1975). Utafiti wake unahusu mwanamke wa Ki-islamu mjini Mombasa, Kenya. Kuhusu ukahaba, anasema kwamba ukahaba ulianza mara tu utumwa ulipopigwa marufuku. Wanawake wengi ambao walikuwa wamewekwa kama masuria na vimada walilazimika kujiingiza katika ukahaba. Pia, watalii na mabaharia waliwaingiza

wasichana wengi katika maisha ya ukahaba. Hata hivyo, kazi hii ya Strobel si ya kifasihi, maana hakuna kazi au vitabu vyovyote vya kifasihi ambavyo amevirejelea. Tena, utafiti wetu haujifungi katika misingi ya kidini.

Utafiti mwingine umefanywa na Little (1980). Little amefanya utafiti wake kuhusu taswira ya mwanamke wa mjini katika fasihi ya Kiafrika. Anajaribu kuonyesha jinsi waandishi wanavyowasawiri wanawake katika maisha ya mjini. Anaonyesha jinsi wasichana wengi upotoka na maisha ya mji na kisha kujiingiza katika ukahaba au mambo ya uasherati na ulevi. Little (1980) amerejelea kazi mbalimbali za fasihi ya Kiafrika zinazomsawiri mwanamke kama kahaba. Hata hivyo, haonyeshi kwa nini maisha ya mjini yanamwaathiri zaidi mwanamke kuliko maisha ya mashambani, hoja ambayo inapata uzito mkubwa katika utafiti wetu.

Pia, Smart (1976) amefanya utafiti wake kuhusu mwanamke na uhuni. Smart ameupatia ukahaba uzito mkubwa katika utafiti wake. Utafiti wake umeanza kwa kuelezea nadharia mbalimbali zinazofafanua ukahaba. Amegusia nadharia ya kisaikolojia na kisosholojia. Isitoshe, ameonyesha jinsi ukahaba unavyoonekana kama suala la wanawake na

si wanaume. Utafiti wake unamtazama mwanamke peke yake kama kahaba wala si mwanamume. Aidha, mtazamo wa Smart (1976) ni kuwa ukahaba ni kitendo cha kuvunja sheria. Kahaba anastahili kuadhibiwa na kufungwa jela. Mtazamo wake ni tofauti na wetu, maana utafiti wetu haushughulikii ukahaba kama kitendo cha kuvunja sheria, mbali ni kazi kama kazi yoyote nyingine yenye umuhimu wa kiuchumi. Tena, utafiti huu wetu unashirikisha wanaume na wanawake kama nguzo katika taasisi ya ukahaba.

Wa aidha, Bakwesegha (1982) ametafiti kuhusu ukahaba nchini Uganda. Bakwesegha anazungumzia jinsi ukahaba unavyoendeshwa mjini Kampala. Katika utafiti huu, Bakwesegha amejishughulisha sana katika kubainisha aina tofauti tofauti za makahaba wanaopatikana mjini Kampala. Pili, ameipatia uzito suala la ni wapi ukahaba hufanyika. Amegusia vilabu vya usiku, vyumba vya pombe na vyuo vya elimu. Isitoshe, ameonyesha athari za 'Mashuga dadi' na 'mashuga mami' katika kuendeleza ukahaba miongoni mwa wanafunzi. Sura ya Mwisho imejikita katika kutambulisha wanaume ambao ni washiriki wa ukahaba. Ameorodhesha aina tofauti tofauti za wanaume, kama vile waliopewa talaka, wale wanaoishi mbali na aila zao na kadhalika. Masuala mengi ambayo yamejitokeza

katika utafiti huu yanapata mtazamo tofauti katika utafiti wetu.

Utafiti mwingine umehaririwa na Muga (1980). Muga amehariri utafiti wa ukahaba uliofanywa Afrika Mashariki, Magharibi,Kusini, Zaire na Nevada. Ama kwa hakika, utafiti huu umemwangalia kahaba kwa marefu na mapana yake. Kwanza umeanzia kwa kuelezea dhana ya ukahaba. Kwa undani zaidi; utafiti huu unajikita katika kutambulisha masuala fulani yanayohusiana na ukahaba kama vile kabila, umri, elimu, dini na uozi. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa hatutajishughulisha na masuala ya umri, kabila, dini na kadhalika. Ijapokuwa kazi ya Muga (1980) inaoneysha mazingira ya mjini, haonyeshi sababu zinazowanasa wasichana na wavulana na kuwafanya makahaba mijini.

## 1.6. MSINGI WA NADHARIA YA UTAFITI.

Nadharia ni kigezo kinachotumika kutathmini jambo. Ukahaba ni suala lenye mawanda mapana sana, kiasi kwamba haliwezi kutathminiwa kikamilifu kwa kutumia nadharia moja. Hii ni kwa kuwa ukahaba husababishwa na hali mbalimbali za kisaikolojia, kisosholojia, kiuchumi na hata kibailojia.

Kutokana na upana huu, nadharia yetu ya utekelezi ambayo tunaitumia kama mizani yetu haitoshelezi bila kuazima kutoka katika nadharia nyingine, hasa nadharia ya kisaikolojia.

Nadharia ya utekelezi imejengeka katika misingi ya elimu-jamii, Lowry (1974:198). Nadharia hii hutazama ukahaba kwa muktadha wa kijamii. Nadharia hii hujishughulisha na dhima na nafasi inayotekelezwa na ukahaba katika jamii. Peck na Coyle katika kitabu chao: How to study literature, literary terms and criticisms (1984) wanasema kwamba nadharia ya utekelezi hutizama jamii kama iliyo na taasisi mbalimbali zinazotekeleza wajibu fulani katika mfumo wa kijamii.

Nadharia ya utekelezi huelezea kwamba ukahaba husababishwa na hali ya kiuchumi. Hivyo basi, ukahaba ni kazi muhimu katika jamii ambayo haina nyanja nyingine za kufanyia kazi. Aidha, nadharia hii inaendelea kuelezea kwamba, ukahaba unaendelezwa zaidi na hali kwamba wanawake wana nafasi chache sana za kazi katika jamii. Kwa nchi ziishizo ulimwengu wa tatu, ukahaba unatekeleza jukumu kubwa sana haswa kwa tabaka la walio chini kiuchumi.

Kingsleys Davis amenukuliwa na Lowry (1974:220) akidai kwamba ukahaba ndiyo taasisi ya kipekee inayohudumia ndoa zisizoridhisha. Wa aidha, taasisi ya ukahaba na taasisi ya ndoa aghalabu hubadilishana majukumu katika jamii.

Kwa hivyo, nadharia hii inafaa sana katika kuhakiki wahusika makahaba katika riwaya za Said A. Mohamed. Hii ni kwa sababu wahusika wengi makahaba wamewajibika kuuza miili yao kutokana na uhitaji wa kiuchumi. Isitoshe, nadharia hii ni mwafaka kunakidi nafasi ya 'mashuga dadi' na 'mashuga mami' katika kuendeleza ukahaba katika jamii. Licha ya hayo, wahusika makahaba wa Said A. Mohamed wanaonyesha mshabaha mkubwa kati ya taasisi ya ndoa na taasisi ya ukahaba.

Kwa upande wa pili, nadharia ya kisaikolojia ya Sigmund Freud (1974) inafaa kuelezea hali mbalimbali za kisaikolojia zinazochangia katika kuwaingiza wahusika fulani katika ukahaba. Huyu mtaalamu wa kisaikolojia anasema kwamba wanawake au wanaume wengi wanaojiingiza katika ukahaba ni wale ambao wana uchu zaidi wa mapenzi. Hali hii huanzia utotoni wakati mtoto anapoanza kumtamani mzazi wake. Ile hali ya kukusanyika kwa uchu pamoja na kuendelea

kupevuka kwa mwili huwafanya watu wengi kuwa makahaba. Watu wenye hii kasoro katika kukua kwao hutumia mapenzi kulipiza kisasi. Zaidi ya hayo, hawawezi kuendeleza mapenzi ya dhati.

Nadharia hii ya kisaikolojia inaonyesha kwamba makahaba wengi hutokana na aila ambazo si imara. Kwa hivyo, makahaba wengi ni wale waliofiwa na wazazi, pamoja na udhaifu wa kupata malezi mabaya. Tumeazimia kupata mchango kutokana na nadharia ya kisaikolojia kwa sababu kuna baadhi ya makahaba katika riwaya za Said A. Mohamed wanaodhihirisha udhaifu wa nafsi kuliko udhaifu wa kiuchumi.

## 1.7. NJIA ZA UTAFITI

Tasnifu hii inahusu sana utafiti wa maktabani. Utafiti huu unahusu kusoma na kuhakiki wahusika makahaba wanaosawiriwa katika riwaya za Said A. Mohamed. Pia, tutasoma riwaya nyingine zenye maudhui ya ukahaba. Hii ni kwa mujibu wa kuongezea nguvu utafiti wetu.

Mwongozo wa utafiti wetu unajikita katika mitazamo ya elimu-jamii na elimu-nafsi. Hivyo inatubidi tusome kazi zinazofafanua taaluma hizi.

Kwa kuboresha utafiti wetu, tutamhoji huyu mwandishi Said Ahmed Mohamed. Mahojiano haya yanachangia sana kuelewa mtazamo wake kuhusiana na wahusika makahaba.

Isitoshe, utafiti huu utahusu kusoma tahakiki mbalimbali ambazo zimeandikwa kuhusiana na riwaya zake Said Ahmed Mohamed. Tahakiki hizi zitatusaidia katika kuelewa maoni ya wanafasihi wengine kuhusiana na maudhui ya ukahaba.

# SURA YA PILI

## 2.0. DHANA NA NADHARIA ZA UKAHABA

Katika sura hii tunajadili mambo kadha wa kadha yanayohusu dhana na nadharia za ukahaba Tunaangalia pia namna mbalimbali za ukahaba na umuhimu wake katika kuelewa ukahaba kwa jumla.

## 2.1. DHANA YA UKAHABA

Shida kuu tunayokumbana nayo tunapopitia kazi yoyote inayohusiana na ukahaba ni maelezo ya dhana ukahaba. Waandishi na wasomi wengi wametoa maelezo yanayokanganya na kuhitilafiana kuhusu maana ya ukahaba. Tofauti hizi zinaibuka kupitia kwa vipenge vinavyoaminika ndivyo hutambulisha kahaba miongoni mwa watu wengine.

Ukahaba ambao unaonekana dhahiri ni ule unaoendelezwa katika madanguro. Ukweli ni kwamba hii ni asilimia ndogo sana ya makahaba maana kuna aina nyingi ya uhusiano tunaoweza kutathimini na kutambulisha kama ukahaba katika jamii zetu. Mathalani, sekretari wakike anapokuwa na mapenzi na 'bosi' kwa matamanio ya kuongezwa mshahara au kupandishwa cheo ni namna fulani ya mtu kujiuza.

Ni wajibu wetu katika tasnifu hii kufanya upembuzi wa namna wahusika mbalimbali wanavyohusiana katika riwaya nne za Said Ahmed Mohamed na jinsi uhusiano wao unavyojikita katika misingi tunayoweza kuiita ukahaba. Hata hivyo, tunaweza kufanya hivyo baada ya kubainisha vigezo muhimu vinavyomtambulisha kahaba katika jamii.

Msomi Dirasse Laketch (1978) alifanya utafiti kuhusu ukahaba. Utafiti wake ulihusu hali ya kijamii na kiuchumi ya wanawake wa jiji la Addis-Ababa, nchini Ethiopia huku akirejelea makahaba. Katika maelezo yake kuhusu ukahaba, Dirasse (1978:15) anasema kwamba:

> "kahaba ni mwanamke au mwanamume anayeshiriki mapenzi na watu wengi kwa matarajio ya pesa au zawadi na bila kuwa na muumano wa kihisia" (tafsiri yetu).

Kufuatana na dondoo hili, Dirasse (1978) amebainisha vigezo vitatu vya kumtambulisha kahaba. Vigezo hivi ni kama vile pesa au faida, kushiriki mapenzi na watu wengi, na kutokuwa na muumano wa kihisia. Wasomi na waandishi wengine ambao wametambulisha vigezo sawa na Dirasse (1978) ni kama vile Muga (1980:25), Bakwesegha (1982:30) na Kishtainy (1982:32). Ama kwa hakika, ni hoja ya busara kufafanua zaidi vipengee hivi huku tukijaribu kutilia maanani namna vinavyoweza kutumika katika kunakidi wahusika katika riwaya za Said Ahmed

Mohamed.

Kigezo cha kwanza ni pesa au zawadi. Hiki ndicho kigezo chenye uzito sana katika kueleza dhana ya ukahaba. Karibu makahaba wote hushiriki mapenzi wakitarajia pesa au zawadi, Chambilecho Kishtainy (1982:32). Kishtainy anafafanua hoja ya zawadi kwa kusema kwamba, mtu anapokubali kuuza mwili ndipo aweze kupata kazi au kupandishwa cheo kazini, basi atakuwa amehiari kufanya kitendo cha ukahaba. Kwa muktadha huu, mwanamke au mwanamume hubadilisha mwili wake kwa faida anayokisia atapata.

Utata unaotokea kufuatia maelezo haya ni kwamba, kuna mahusiano mengi katika jamii zetu yanayojikita katika misingi ya kifedha au faida na hatuyaiti ukahaba. Mathalani, usuria. Katika usuria, mwanamke hukaa na mwanamume kwa muktadha kwamba huyu mwanamume atayakimu mahitaji yote ya kiuchumi ya huyo nwanamke ilihali mwanamke atatosheleza mahitaji ya mwanamume, yakiwepo tamaa zake za kimwili (Strobel: 1975:50). Hoja nyingine sawa na hii imezushwa na Engels (1944). Engels adai kwamba ndoa nyingi zinazoendelezwa katika jamii za kimwinyi na kibepari huwa ni kiwango fulani cha kahaba maana wanawake wengi huwakubali wanaume fulani kwa vile ni matajiri. Uhusiano wao umejengeka katika misingi ya kifedha.

Katika mataifa ya ulimwengu wa tatu, maisha ya kiuchumi ni ya kutegemeana. Wanawake wengi hawajafikia kiwango cha kujisimamia kiuchumi. Hii ndiyo sababu hali ya usuria na ndoa za kununuliwa ni nyingi sana. Isitoshe, katika muktadha wa jamii za Kiafrika, uhusiano wa aina hii haujashtumiwa na kuitwa ukahaba. Hii ni labda ni kwa vile ni hali halisia kuwa wote wawili hawangeishi vizuri kama wangekuwa hawana uwezo wa kiuchumi.

Kwa kiwango hiki, tumekubaliana kwamba ukahaba ni kitendo cha mwanamke au mwanamume kushiriki mapenzi na mwenzake kwa matamanio ya kufaidika kihali na mali. Aghalabu, uhusiano wa hawa watu wawili huisha mara tu kitendo kinapokamilika. Kwa hivyo ukahaba ni aina fulani ya biashara. Biashara ya aina hii hujidhihirisha dhahiri shahiri kwa makahaba tunaowapata katika madanguro.

Ni kutokana na uhitaji wa kiuchumi ndipo wasichana fulani huweza kujisalimisha kimapenzi kwa watu wenye uwezo wa kuajiri kazi, Chambilecho Mbilinyi (1982:23).

> "Wasichana wengi ambao ni wahitaji
> wa kazi wanakabiliwa na tatizo
> kubwa kutoka kwa wanaume, wanao-
> walazimisha kujiuza ndipo
> wapate kazi" (tafsiri yetu).

Kwa muktadha huu, msichana hulazimika kuuvunja utu wake na kujisalimisha kwa matumaini ya kazi. Kitendo chake ni kitendo cha ukahaba, maana ameubadilisha mwili wake na kazi au cheo ambacho atapata au ameishapata. Maelezo ya Emmanuel Ngara Art and Ideology (1985:56) katika tahakiki yake ya riwaya ya David Mailu After 4.30 (1974) anasema kuwa wasichana wengi wanaokataa njama za 'mabosi' wao huishia katika lindi la kuachishwa kazi.

Ni kutokana na hiki kigezo cha pesa ndipo uhusiano wa 'akina mama' na 'akina baba' matajiri na vijana wabichi huhesabiwa kama ukahaba. Bakwesegha (1982:8) anasema kuwa:-

> "Wanawake au wanaume matajiri wanaowakimbiza vijana wabichi kwa nia ya kutosheleza tamaa zao za kimwili hudhihirisha hali ya ukahaba zaidi ya uasherati (tafsiri yetu).

Maoni yetu yanaafikiana na haya ya Bakwesegha maana hawa akina mama na baba, hutumia pesa kununua hawa vijana wabichi. Wa aidha, hawa vijana wanaonunuliwa pia ni makahaba kwa sababu wanakubali kuvunja utu wao na kujiuza. kwa minajili ya pesa. Hiki kitendo cha mtu kuuza mwili wake kwa pesa ni kitendo cha kuvunja utu katika jamii nyingi za Kiafrika.

Kigezo cha pili cha kumtambulisha kahaba ni uasherati. Uasherati ni hali ya mtu kushiriki mapenzi

na watu wengi. Hoja ya makahaba kuwa na wateja wengi sana ni hoja ya kweli na si kweli. Hali hii hutegemea tabaka la kahaba mwenyewe. Ni kweli kwamba makahaba wengi hawana uchaguzi, mradi tu mteja awe na pesa. Wa aidha, si lazima mtu kushiriki mapenzi na watu wengi ndipo tumwite kahaba. Uhusiano hata uwe wa watu wawili au zaidi, kilicho muhimu ni nia ya mtu kwa mwenzake. Little (1973:114-120) anasema kuwa makahaba wa tabaka la juu aghalabu hujihusisha na mpenzi maalamu mwenye hadhi fulani, kama vile kiongozi, wanafalsafa na wanasiasa.

Hoja ya kutahadharisha hapa ni kwamba tusichukulie uasherati kwa ujumla kumaanisha ukahaba. Uasherati ambao ni ukahaba ni ule wenye mizizi ya matamanio ya pesa. Hii ndiyo nguzo kwa makahaba wa tabaka la chini wanaopatikana katika madanguro na vichochoroni. Uasherati ambao si ukahaba ni ule wa kuridhisha nafsi. Wavulana na wasichana wengi aghalabu huwa na wapenzi wengi lakini hatuwezi kuwatia katika kijopo cha makahaba. Hii ni kwa vile azimio lao si kufaidika bali ni kutambulisha uume na uke wao.

Kigezo kingine cha kumtambulisha kahaba ni ile hali ya kutokuwa na mshikamano wa kihisia. Twafahamu kwamba 'mapenzi' ya makahaba huwa hayana muumano wa kihisia.

Uhusiano wao ni uhusiano wa chombo kwa chombo. Sote tunajua kwamba chombo hakina hisia na huendeshwa na mfumo ulio na nguvu. Kitovu cha uhusiano wa kahaba na mteja wake kiko pale kwenye kitendo na faida yenyewe. Hakuna mapenzi ya dhati.

Shida inayojitokeza na hoja hii ni kwamba ni vigumu sana kutathmini hisi za mtu. Smart (1976:77) anadai kuwa makahaba hawawezi kuwa na mshikamano wa kihisia kwa vile nguzo kuu ni fedha. Tunachoweza kusema ni kuwa, kigezo hiki kilichopendekezwa na Dirasse (1978), Muga (1982) na wengine kinaweza kunakidiwa katika kazi ya fasihi kupitia maelezo ya kisaikolojia ya wahusika.

Kutokana na mjadala huu, inabainika kwamba ukahaba ni taasisi inayojumulisha wanawake na wanaume tofauti na mtazamo wa kimapokeo, Chambilecho Smart (1976:62):

> "Mtazamo wa kimapokeo ulihusisha ukahaba na wanawake peke yake na kuwatenga wanaume" (tafsiri yetu).

Hoja hii ya kimapokeo ilipata uzito kutokana na hali kwamba ni rahisi kumtambua kahaba wa kike kuliko kahaba wa kiume. Wa aidha, wanaume walijitambulisha katika jamii kupitia kwa namna wanavyoweza kushiriki mapenzi na wanawake wengi. Kwa upande wa kike, ni kinyume chake

maana mwanamke alipaswa kuwa 'msafi' kimapenzi mpaka siku ya kuolewa (Smart: 1976: 63).

Katika tasnifu hii, mtazamo wetu ni kuwa ukahaba ni taasisi nayohusisha wanaume na wanawake. Wote ni washiriki, na tasnifu yetu haingeonyesha ukamilifu wowote kama tungeshughulikia makahaba wa kike peke yake, chambilecho Mailu (1974:9):

> "Kama wanawake ndio makahaba pasi tungeshindwa kueleza wanafanya huo ukahaba na nani... Makahaba wengi wa kiume hawafikiri kama wao ni makahaba". (tafsiri).

Wanawake wamekuwa wakionekana kama makahaba kutokana na taasubi za kiume zinazomdhalilisha na kumtazama mwanamke kama chombo cho kumfurahisha mwanaume.

Dhana ya ukahaba inaweza kutizamwa kama kitendo au tabia ya mtu kuuza mwili wake ndipo aweze kufaidika. Ni kama biashara, ambapo anayehusika hujinadi kwa madhumuni ya faida. Ukahaba unaweza kujitokeza kama uhusiano. Uhusiano huu hujengeka katika misingi ya mapenzi yasiyo ya dhati na mtu hutumia uhusiano huo kujichumia.

Nguzo muhimu za ukahaba ni faida na starehe. Hali ngumu ya kiuchumi ndiyo huzaa watu wanaohiari kuuvunja

utu wao kwa kujinadi mabarabarani. Ukahaba ni kitendo au uhusiano wa watu wawili. Wote ni washiriki. Hivyo basi kuna 'kahaba na mteja'. Katika uhusiano au kitendo chao, kila mmoja huridhika. Mteja huridhisha nafsi yake baada ya kupata alichokihitaji. Naye muuzaji (kahaba) hunufaika kwa kupata mali au faida yake.

## 2.2.0. NADHARIA ZA UKAHABA

Mada zote za utafiti, ukahaba ukiwa mojawapo aghalabu huhitaji kuwa na msingi wa kisayansi. Misingi ya kisayansi huwa ni vigezo vya kutathmini kazi. Wataalamu wamezua nadharia mbalimbali zinazoelezea kuweko kwa ukahaba katika jamii.

### 2.2.1. NADHARIA YA UPEMBUZI WA NAFSI

Mwanasaikolojia maarufu Sigmund Freud ameelezea maisha ya ukahaba katika nadharia aliyozua ya Upembuzi wa nafsi. Freud (1974) amefanya utafiti wake kuhusiana na hali ya ukahaba na uasherati. Freud (1974) alijishughulisha na masuala ya kwa nini mtu kuwa kahaba na kama tabia hii ni ya kawaida au la.

Nadharia ya upembuzi wa nafsi imehakikiwa na kuendelezwa na wataalamu wengine kama vile Robey

katika kitabu chake. Modern Literary theory (1982) Robey anasema kuwa nadharia hii hujihusisha na hali ya kisaikolojia ya mhusika katika kazi ya fasihi. Wa aidha, nadharia hii huendeleza masuala fulani yanayohusiana na nafsi ya mhusika. Ni kweli kuwa makahaba hudhihirisha udhaifu fulani wa nafsi.

Freud (1974) amenukuliwa na Smart (1976:50) akidai kwamba hali ya ukahaba huanzia utotoni, wakati ambapo mtoto huanza kujitambulisha kimapenzi na mzazi wake. Mtoto wa kike huanza kumtamani baba, naye wa kiume humtamani mama. Kwa vile hakuna chochote ambacho kinaweza kuendelea kati ya baba na mwana, hali ya chuki na kutopendana huanzia.

Jinsi mwili wa mtoto unavyozidi kupevuka ndivyo uchu wa kimapenzi unavyozidi kukusanyika. Punde tu afikiapo kiwango cha utu uzima ambapo anapata nafasi za kuingiliana kimapenzi na wenzake, ukahaba na uasherati huanzia kama njia ya kutosheleza uchu wake wa siku nyingi.

Maelezo mengine kuhusiana na hii nadharia ni kwamba, ile hali ya mtoto kumchukia mzazi huendelea hadi utu uzima. Aghalabu, mtu anapokuwa na chuki na mwenzake hutafuta mbinu zote za kumwadhibu. Njia ya kipekee ya

huyo 'mtoto' kumwadhibu anayemchukia ni kupitia kwa mapenzi. Huyu msichana au mvulana humwadhibu mwenzake kwa kumpatia mapenzi yasiyo ya dhati. Mapenzi ambayo hayana ule moyo wa undani. Hii huwa ni njia moja ya kulipiza kisasi kwa mapenzi waliyonyimwa.

Kwa mkururo huo huo wa maelezo, mtoto ambaye hakutoshelezwa matakwa yake ya kimapenzi huanza kufikiria kwamba mzazi wake hampendi; hana mapenzi ya uzazi kwake. Kutokana na mawazo hayo, msichana au mvulana huyu anapokua, hujaribu awezavyo kutafuta mapenzi aliyoyapoteza kupitia kwa watu wengi. Kwa hivyo kupitia kwa ukahaba yeye hufikiria anapendwa na watu wengi. Hii ni mbinu ya kutosheleza nafsi ya mtu.

Kufikia kiwango hiki, tumeona kwamba mtoto ambaye hupatwa na 'kasoro' hii huendelea na huwa na tabia ya kitoto hadi utu uzima. Watu kama hawa kwao ni shida sana kuanzisha mapenzi ya kawaida ambayo yamekomaa na yanayoweza kudumu.

Ama kwa hakika, maelezo yote ambayo tumetoa kuhusu nadharia hii yanatumulikia dhana kwamba kahaba ni mtu ambaye hajakomaa kihulka. Kifikira, makahaba ni watu ambao wana kasoro katika maisha yao. Kasoro katika kukua kwa nafsi zao.

Mitazamo mbalimbali ya kisaikolojia imehusishwa na kuweko kwa ukahaba. Mtaalamu Daktari Rutasitara ananukuliwa na Muga (1980) akisema kwamba makahaba wengi hutokana na familia zisizo imara. Labda wazazi

wametengana au hawaishi kwa amani. Rutasitara alifanya utafiti wake mjini Mombasa miaka kumi iliyopita na ametambulisha kwamba zaidi ya asilimia sitini ya makahaba huwa wanatokana na aila zilizovunjika. Maelezo sawa na haya yalielezwa na Smart (1976).Hali ya wazazi kutengana, kufa au kutoishi kwa ushirika huleta malezi mabaya pamoja na madhara mengi ya kiuchumi.

Mintarafu ya utafiti wake Rutasitara, ametambulisha kwamba makahaba mia moja na sabini na wane kutokana na makahaba mia mbili aliowahoji walijiiza katika kazi hii kwa vile ni kazi rahisi na haina mahitaji mengi. Kwao, sababu za kiuchumi si muhimu. Wanataka kuridhisha nafsi zao kwa kufanya kazi ya uzembe. Hata hivyo, mtaalamu mwingine Kingsley Davis amenukuliwa na Lowry (1974:201) akipinga hoja ya Rutasitara kwa kusema kwamba:

> "Ukahaba ni kazi ngumu na ya kinyaa. Malipo ya kahaba huwa si tunu kwa kazi yake au ujuzi wake bali ni kulipa hadhi na utu ambao ameupoteza katika jamii" (tafsiri yetu).

Mtu anapouza mwili wake, hujivunjia utu na hadhi katika jamii. Jamii nyingi za Kiafrika humtazama kahaba kama mhuni au mwasi. Hivyo, kazi ya ukahaba siyo ya kujivunia bali ni ya kujivunjia hadhi na heba.

Kufikia hapa, hatuna budi kutathamini uzito na upungufu wa hii nadharia ya saikolojia. Upungufu wa kwanza unaojitokeza ni kwamba Sigmund Freud alikichukulia kipengee cha uasherati kuwa ni ukahaba. Hoja yake si

makosa lakini ni dhaifu bila kujengwa na kipengee cha pesa au faida. Uasherati peke yake hatuwezi kusema ni ukahaba.

Upungufu mwingine wa hii nadharia ya kisaikolojia ni kwamba ni vigumu sana kupima saikolojia ya mhusika katika fasihi. Tunapofanya hivyo huwa tunakisia tu yale ambayo labda yanaendelea katika akili yake. Ama kwa hakika, ni vigumu sana kusema huyu mhusika amejiingiza katika ukahaba kwa minajili ya kulipiza kisasi kwa mapenzi aliyonyimwa na mzazi. Hali hii ya kihisia hufichika katika mhusika. Ni chembe chembe kidogo ambazo zinaweza kujitokeza.

Hata hivyo, nadharia hii ina uzito wake katika kutathmini baadhi ya wahusika tunaowapata katika kazi za fasihi. Mathalani, ni kweli kwamba watu wengi hujiingiza katika ukahaba kutokana na hali kuwa familia zao si imara. Kwa hivyo, unyonge wa nafsi, fikira na hisia ndio huwavuta katika ukahaba. Wa aidha, hali hii huleta malezi baya na unyonge wa kiuchumi.

Aghalabu, makahaba na wateja wao huridhisha nafsi zao. Hali hii ya kuridhisha nafsi ni muhimu sana katika uteuzi wa kazi au tabia. Mwanamke anapopewa talaka, au kuzaa nje ya ndoa si lazima aanze kujinadi. Mvulana anapokuwa hajiwezi kimali si lazima ajirahishe kwa akina

mama wenye mali. Wote hufanya hivyo kutokana na hali fulani za kihisia na mwelekeo.maana kuna kazi nyingine wangefanya. Nafsi zao ndizo mwongozo.

2.2.2. NADHARIA YA UTEKELEZI

Nadharia ya utekelezi ni miongoni mwa nadharia nyingi zenye mtazamo wa kisosholojia. Nadharia ya utekelezi imeendelezwa sana na wanasosholojia kama vile Talcort Parsons na Emile Durkheim kama wanavyonukuliwa na Worsely - Introducing Sociology (1970). Hawa wanasosholojia wanasema kuwa nadharia ya utekelezi hujishughulisha na jukumu linalotekelezwa na taasisi mbalimbali za jamii kwa madhumuni ya maendeleo ya jamii kwa jumla.

Kwa mtazamo wa kifasihi nadharia ya utekelezi imehusishwa sana na nadharia ya miundo. Peck na Coyle katika kazi yao How to study literature, literary terms and criticisms (1984) wanasema kuwa mtazamo wa nadharia hizi mbili si tofauti maana zote hujishughulisha na jamii kama mfumo mmoja uliogawika katika viungo vingi vinavyofanya kazi kwa pamoja. Kila kiungo kina nafasi na dhima ya kutekeleza katika jamii. Nadharia hizi hujali sana umbo la kazi fulani, uchoraji wa wahusika na umbuji wa mwandishi kwa jumla.

Katika kipindi cha karne ya kumi na tisa, utafiti wa kisosholojia ulifanywa na Parent Du Chatelet (Smart: 1976) kuhusiana na mada ya ukahaba. Utafiti huu wa kisosholojia ulitambulisha kwamba ukahaba unasababishwa na hali ya kiuchumi. Hivyo basi, ukahaba unatekeleza jukumu muhimu la kiuchumi katika jamii. Bakwesegha (1982) anaendeleza dhana hii kwa kusema kwamba wanawake wengi wanaoishi katika mataifa ya ulimwengu wa tatu hujiingiza katika maisha ya ukahaba kutokana na hali ngumu ya kijamii na kiuchumi.

Kingsley David ambaye ni mwana sosholojia mwenye mtazamo wa kiutekelezi amenukuliwa na Lowry (1974:220) akieleza kwamba katika jamii ya kisasa, kuna sababu kadha wa kadha zinazoelezea kuwepo kwa ukahaba. Kwanza, ukahaba husababishwa na ile hali ya kutaka kujinufaisha kifedha pamoja na hali ya kuridhisha nafsi. Davis, anaendelea kusema kuwa mapenzi huuzwa katika miktadha mbalimbali ya kijamii. Mathalani katika ndoa, katika usuria na katika mashindano ya urembo. Hata hivyo miktadha hii haijahesabika kama ukahaba, maana viwango vya matumizi yake ni tofauti.

Davis (Lowry 1974: 224) anaendelea kudai kwamba ukahaba ni taasisi inayohusiana sana na taasisi nyingine kama vile ndoa na kadhalika. Watu wengi ambao hawaridhiki

na ndoa zao aghalabu hupata mapenzi nje ya ndoa kupitia ukahaba:

> "Ukahaba katika jamii za kisasa kutekeleza wajibu muhimu wa kiuchumi na ndiyo njia ya kipekee ya kutosheleza mahitaji ya kimwili ya watu wenye ndoa zisizo na misingi imara (tafsiri yetu).

Kufuatana na dondoo hili, ukahaba ni chombo kitekelezi katika kuendeleza jamii. Jamii inayo viungo vingi lakini vinauhusiana, mathalani ukahaba na ndoa. Kwa hivyo ukahaba utekeleza wajibu muhimu sana maana ni namna ya kuchuma, pili utekeleza jukumu la kutosheleza mahitaji mengi ya kimwili ambayo hayawezi kutekelezwa na taasisi nyingine katika jamii. Kwa hivyo ukahaba una nafasi kubwa sana katika ndoa za mke mmoja mme mmoja.

Davis katika nadharia yake ya utekelezi (Lowry: 1974: 118-224) anawashtumu wale wataaalamu wenye mtizamo wa kimaadili. Wataalamu hawa hudai kwamba ukahaba ni dhambi na ni uhuni, Hivyo unastahili kukomeshwa. Pia, anawakashfu wanasayansi wanaodai kwamba ukahaba unastahili kukomeshwa maana husababisha magonjwa ya zinaa. Davis, anasema kuwa ukahaba hausababishi magonjwa; magonjwa husababishwa na uasherati pamoja na matumizi ya mapenzi holelaholela.

Maoni ya Davis (Lowry: 1974: 120), Finnegan (1979) na Muga (1980) yanashabihiana. Wote wana wazo kuwa jamii za kisasa zinauhitaji mkubwa sana wa ukahaba. Hoja ni kwamba watu wengi siku hizi hufanya kazi mbali na jamaa zao. Kazi kama vile uanajeshi, ubahari na kadhalika. Wote hawa huhitaji huduma kutoka kwa makahaba. Isitoshe, watu wengi ambao ni vilema huweza kutosheleza tamaa zao za kimwili kupitia kwa ukahaba.

Nadharia ya utekelezi inashikilia kwamba ukahaba ni hali ya kimaisha inayosababishwa na hali ya uchumi wa jamii pamoja na ile hali ya kutaka kuridhisha nafsi kwa mbinu za ubinafsi. Ukahaba hauna suluhisho rahisi katika jamii. Labda jamii inahitajika kuwa na mabadiliko yatakayoruhusu hali nzuri ya kiuchumi pamoja na ndoa zenye uaminifu na usawa.

Nadharia hii ina uzito mkubwa katika kufafanua taasisi ya ukahaba. Ni dhahiri kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya ndoa na ukahaba. Zote ni taasisi zinazochangiana kwa namna moja ama nyingine. Maana watu wengi huweza kutoka katika taasisi ya ndoa na kujiingiza katika ukahaba au kutoka katika ukahaba na kuingia katika ndoa. Vile vile ndoa nyingi hutoshelezwa na ukahaba.

Isitoshe, nadharia hii ina mtazamo kwamba ukahaba husababishwa na hali ya kiuchumi pamoja na hali ya kuridhisha nafsi. Hoja ambayo tumeafiki ni ya kweli. Hali ya kutaka fedha au kuridhisha nafsi ni uhitaji na uhitaji hauna kipimo. Maana matajiri huwa na uhitaji wao sawa na maskini. Hivyo nadharia hii inafaa katika kuelezea ni kwa nini wanawake na wanaume matajiri hushiriki katika ukahaba sawa na wafanyavyo makabwela. Wa aidha, nadharia hii inahusisha ukahaba na jamii. Nadharia hii inaweza kuwa mwongozo mzuri katika kuhakiki wahusika makahaba katika kazi ya fasihi.

## 2.2.3. NADHARIA YA KI-MARX.

Nadharia ya Ki-Marx hujaribu kuelezea athari za kiuchumi katika mfumo wa kijami wa wakati fulani katika historia na pia husisitiza ufafanuzi wa mitafaruku ya kitabaka. Mitafaruku hii hujitokeza kutokana na sababu za kisiasa na kiuchumi. Arvon katika kazi yake Marxist aesthetics (1978:XIV) anasema kwamba nadharia ya ki-Marx:

> "Hujaribu kudhihirisha uhusiano uliopo kati ya mifumo ya kisiasa na uchumi na jinsi uhusiano huu unavyoathiri maendeleo ya jamii" (tafsiri yetu).

Kulingana na nadharia ya Ki-Marx, ukahaba umejitokeza zaidi katika jamii kutokana na kuanzishwa

kwa maisha ya viwandani yaliyoathiri muundo wa jamii sana. Jamii ilibadilika na matabaka yakapata nguvu. Haya matabaka yalitokana na ule uhitaji wa kiuchumi ambao ulianza kuongezeka. Matabaka haya yalifungamana na kugawa kazi kulingana na uana. Mfumo huu wa maisha ya viwandani uliwaathiri sana wanawake. Kutokana na uhitaji mkubwa wa kiuchumi, wanawake wengi walianza kukimbilia mijini kutoka mashambani kwa minajili ya kazi, chambilecho Kishtainy: 1982:46).

> "ukahaba kulingana na Marx ni kazi muhimu inayotajariwa chini ya mfumo wa maisha ya viwandani". (tafsiri yetu).

Uzito kutokana na dondoo hili ni kwamba baada ya kazi za viwandani kugawanywa kulingana na uana, wanawake wana nafasi chache sana za kazi katika jamii.

Hoja dhahiri inayojitokeza kulingana na nadharia hii ni kuwa, ukahaba ni kiwakilishi cha kukandamizwa kwa tabaka la wanyonge katika jamii (Dirasse: 1981). Kwa mtazamo huu, ukahaba ni suala la wanawake wote katika jamii, yaani kuonewa huku kwa mwanamke hadi kufikia ukahaba chanzo chake kimetokana na mfumo wa ubepari (Kishtainy: 1982:46).

Kulingana na mtazamo wa Ki-Marx, ubepari uliambatana na binadamu kunyimwa haki na mahitaji na

binadamu mwenzake. Kutokana na uhitaji wa kiuchumi binadamu walianza kuuza nguvu na miili yao kutokana na uhitaji. Umuhimu wa kitu ukawa ni thamani yake baada ya kuuzwa. Kwa kuitikia mwito wa kiuchumi, ukahaba ukajitokeza.

Wanawake kama wafanyikazi wa viwandani ni watu ambao wakandamizwa kiuchumi, kwa hivyo ukombozi wao utaandamana sambamba na ukombozi wa wafanyikazi. Hivyo basi ukahaba kuambatana na maoni ya Marx na Engel (1966) ni zao la mfumo wa ubepari.

Maoni ya Kishtainy (1982:30), Finnegan (1979) na Engels (1944) ni kuwa wateja wengi wa makahaba ni mabepari na mamwinyi. Wale wenye uwezo wa kiuchumi. Tena ni wakati wa mifumo ya Umwinyi na kibepari ndipo wanawake walitawishwa. Hali hii iliwezesha wanaume kuwa na wapenzi wengi nje ya ndoa. Hali hii iliuinua ukahaba sana katika jamii zilizohusika.

Nadharia hii ya Ki-Marx inasisitiza sana ubepari kama ndicho chanzo cha ukahaba. Hii ni hoja isiyo na mashiko. Ukahaba una historia defu sana katika jamii. Ukahaba ulitumika huko Ugiriki katika Mahekalu takatifu (Kishtainy: 1982). Hata jamii za kikomunisti ukahaba hupatikana (Lowry: 1974).Ubepari si chanzo cha ukahaba, lakini uliinua juu mpaka ukaanza kujitokeza kwa uwazi

kama mbinu ya kujiendeleza kiuchumi .

Upungufu wa pili wa nadharia ya Ki-Marx unaonekana kupitia kwa mtazamo wake kwamba tusimchukulie kahaba kama mtu binafsi, bali tuwaangalie kama kundi ambalo limeonewa, chambilecho (Kishtainy (1982:8):

> "Makahaba wa kike katika fasihi ni kiwakilishi cha maovu yote ya ubepari, yakiwepo kunyanyaswa kwa wanawake na wanaume". (tafsiri yetu).

Ama kwa hakika, si kweli kwamba makahaba wote ni wa tabaka la chini. Kuna wale wa tabaka la juu na wale wa tabaka la chini. Makahaba wa tabaka la juu hatuwezi kusema wananyanyaswa. Aghalabu, wao ndio wanaonyonya kutoka kwa matajiri. Kwa kuongezea nguvu hoja hii, Kishtainy (1982:42) anasema:

> "Wanawake wengi wajiingiza katika kazi ya ukahaba maana mapato yake ni nafuu kuliko kazi ya ofisini... hali ya kiuchumi ya kahaba ukilinganisha na dadake ambaye si kahaba daima huwa nzuri. (tafsiri yetu).

Dondoo hili linatuonyesha namna ambavyo wanawake katika mataifa yaliyostawi wanavyofurahia ukahaba. Bakwesegha (1982:3) anaendeleza hoja hii kwa kusema kuwa alihamasishwa kutafiti kuhusu ukahaba kutokana na idadi kubwa ya wanawake na wanaume walioelimika ambao wanajiingiza katika maisha ya ukahaba.

Baada ya kunakidi nadharia mbalimbali zinazofafanua hali ya ukahaba, hatuna budi kuamua ni nadharia ipi au zipi tutakazofuata kama mwongozo wa utafiti wetu. Katika maelezo yetu kuhusu dhana na nadharia za ukahaba, tumeona kwamba ukahaba una mawanda mengi sana.

Msingi wa nadharia ya utafiti wetu unajengeka katika nadharia ya utekelezi. Hii ni nadharia yenye mtazamo wa kisosholojia. Hata hivyo, haitaweza kutosheleza mahitaji ya hii tasnifu bila kuanzima machache kutokana na nadharia ya kisaikolojia. Imetubidi kuhusisha nadharia mbili kutokana na hali kwamba wahusika makahaba wanaopatikana katika riwaya za Said Ahmed Mohamed wanadhihirisha hali mbalimbali za ukahaba zenye mitazamo mbalimbali. Ukahaba ni suala la kijamii, suala la kiuchumi pamoja na kuwa ni suala la kisaikolojia.

Tunachosema hapa ni kwamba hatuwezi kunakidi kikamilifu usawiri wa mhusika kahaba katika fasihi bila kumhusisha na hali ya jamii. Tena ni lazima tumtazame huyo mhusika kama mtu binafsi, mwenye hisia na mwelekeo fulani.

Ukahaba katika mataifa ya ulimwengu wa tatu, husababishwa na hali mbaya za kiuchumi. Hali hii mbaya husababishwa na hali mbalimbali za kijamii. Hivyo, nadharia ya utekelezi itatusaidia katika kumtazama binadamu katika mazingira yake ya kijamii. Mathalani, itatusaidia kuona uhusiano uliopo kati ya ndoa na ukahaba.

Katika utangulizi wa nadharia ya utekelezi, tulisema kwamba nadharia hii hujihusisha na wajibu unaotekelezwa na viungo na taasisi mbalimbali za jamii. Hivyo basi, tutaweza kutumia nadharia hii kutathmini jukumu la ukahaba. Zaidi ya hayo, hatuna budi kuangalia namna wahusika makahaba wanavyoondoshwa kutoka katika maisha haya. Ni wajibu wetu kunakidi jukumu linalotekelezwa na ndoa, kifo na hali ya kurudi mashambani kama suluhisho la ukahaba. Hivi vyote ni vipembe vya jamii na vina wajibu wake katika mfumo wa maisha ya jamii.

Nadharia ya utekelezi ina mtazama binadamu kama mhitaji. Kuna aina mbili kuu za uhitaji. Uhitaji wa kicuhumi na uhitaji wa kuridhisha nafsi. Hivyo basi nadharia hii ya utekelezi inafaa sana

katika kuelezea kwa nini ukahaba huendelezwa na watu wa tabaka zote; matajiri na hata makabwela.

## SURA YA TATU

### 3.0. WAHUSIKA MAKAHABA NA SABABU ZINAZOWAVUTA

Fasihi inajukumu la kumulika uhalisia katika jamii. Wanafasihi huelezea matatizo na mafanikio ya jamii kama wanavyoyaona kulingana na tajriba zao. Mwandishi huyafichua matatizo na mafanikio ya jamii kwa kuyaweka katika lugha iliyo wazi na yenye kueleweka. Waandishi wa Fasihi hutumia lugha kuweza kutoa fikra, rai na falsafa zao wakizingatia wahusika ambao wanawaweka katika mazingira yanayostahili kwa msomaji huku wakiwa na lengo la kuzua hisia tofauti na mafundisho muhimu. Wahusika hawa huzaliwa kutokana na maisha halisi ya jamii.

Wanafasihi wengi wa karne ya ishirini akiwemo Said Ahmed Mohamed wanatusawiria jamii zinazosheheneza ubinafsi, ufisadi na tadi. Hali hii imewaacha wengi wakitambana njia kwa madhumuni ya kuyaendeleza maisha yao kama asemavyo Hower (1970:25). Kwa hivyo, uhusiano wa binadamu kusaidiana na binadamu mwenzake bila kuthamini faida umefifia.

Wale wenye uwezo wa kiuchumi na kisiasa wamejirundikia elimu bora, kazi bora na vyeo vikubwa. Wale duni, makabwela, wanaelea

hewani kama tiara. Wanachezea kule angani kwa madhumuni ya kumfurahisha mwanadamu, haswa mwenye kujikimu kiuchumi. Punde tu uzi unapokatika, tiyara itaweza kupelekwa popote na upepo. Hawa wahitaji wanasukumwa na mkondo wa kiuchumi. Tunaelewa kwamba 'Mhitaji ni mtumwa'. Uhitaji umewafanya wasichana na wavulana wengi kuutupa utu na kuuza miili yao kwa yeyote aliyetayari kununua.

Said Ahmed Mohamed ameendeleza hali ya uhitaji vizuri sana katika riwaya zake. Wa aidha, ameonyesha kwa mawanda marefu uhitaji wa kiuchumi unaowakabili wengi katika jamii ya Unguja na Afrika Mashariki kwa jumla. Katika kuendeleza uhitaji huu Mohamed ametalii vizuri sana taasisi ya ukahaba. Ametusawiria baadhi ya wahusika wake kama makahaba kutuonyesha jinsi muundo wa jamii unavyoathiri nyanja za kiuchumi.

Taasisi ya ukahaba ina mawanda mapana sana kiasi kwamba hatuwezi kuyatizama yote kwa pamoja. Wahusika makahaba katika riwaya nne za Said Ahmed Mohamed wanaweza kugawika katika majopo mawili. Jopo la kwanza linahusu wahusika wanaoendeleza maisha yao kwa kutumia mbinu ya kuuza miili yao. Jopo la pili linahusu wahusika wanaosawiriwa wakihusiana kwa misingi ya kifedha au faida, kigezo ambacho

tulisema ndiyo nguzo kuu ya kutambulisha ukahaba. Kwa muhtasari, tunachosema hapa ni kwamba Said Ahmed Mohamed ametusawiria taasisi ya ukahaba kama biashara, tena ni uhusiano. Tutawahakiki wahusika hawa huku tukiwa na madhumuni ya kutambulisha sababu zinazowaingiza katika mfumo wa ukahaba.

Kabla hatujaingilia uhakiki wetu, sharti ifahamike kwamba tunatathimini kigezo cha unyonge kama kiini cha ukahaba. Unyonge kwa muktadha huu unatumika kuonyesha unyonge wa kiuchumi na unyonge wa nafsi. Aghalabu, unyonge wa kiuchumi huenda sambamba na unyonge wa nafsi. Isipokuwa kuna nyakati fulani ambapo unyonge wa nafsi huwa huru. Mathalani, mtoto wa aila ya kifalme anapotawishwa, huwa ana unyonge wa nafsi lakini hana unyonge wa kiuchumi.

### 3.1.1. WAHUSIKA WANAOCHUMA KWA KUUZA MIILI YAO.

Riwaya za Said Ahmed Mohamed zinatupa picha ya mfumo wa kimwinyi. Mfumo wa kimwinyi ni mfumo wa kitabaka ambao umetawaliwa na ubinafsi. Kwa muktadha huu, wanawake na wanaume fulani waliwajibika kuutupa utu na kuuza miili yao ndipo waweze kujipatia riziki. Mulokozi (1982:42) anasema kuwa mfumo huu wa kimwinyi ulimdunisha mwanamke sana mbele ya mwanamume.

Katika kutimiza lengo letu la sehemu hii, tumechagua kuwahakiki wahusika wafuatao; katika Asali Chungu hatuna budi kunakidi usawiri wa mhusika Semeni na Pili. Katika Utengano tutajishughulisha na mhusika Maimuna. Uteuzi huu hauna maana kwamba hakuna wahusika wengine wanaochuma kwa kuuza miili yao. Katika Utengano, msanii ametutajia wahusika wengine kama vile Kijakazi na Dora, Katika Asali Chungu, kuna wahusika kama vile Riziki, Maulidi na Naima. Kuwateua Maimuna, Semeni na Pili kama kiwakilishi chetu ni kwa sababu wahusika hawa wamepewa maelezo marefu ukilinganisha na wale wengine. Hivyo, watatuwezesha kufikia malengo yetu.

Katika Asali Chungu, tunakutana na mhusika Semeni. Semeni alifumwa na msiba wa kufiwa na mamake akiwa mtoto. Babake akatoweka utoroni kusikojulikana. Maisha ya mashambani yalimshinda kwa kukosa muhisani. Pale mashambani, maisha yalikuwa magumu sana, kiasi cha kwamba alianza kuombaomba. Kutokana na hali hii, alihamia mjini alikofikiria atajipatia riziki yake.

Kuhusu usawiri wa Semeni, msanii ana mtazamo wa kitanzia. Hii ni ile imani ya majaliwa. Mtazamo wa kitanzia unaonekana kupitia kwa hoja kwamba Semeni

kazaliwa katika mateso na akafa katika mateso. Katika malezi ya Semeni, tunaonyeshwa kifo cha mamake, Maua, na kutoroka kwa babake. Hili ni tukio la hatari na masikitiko makubwa kwa malezi ya Semeni. Baada ya kifo cha wazazi wake, Semeni alimpata Bi Mtama kama mlezi wake. Punde si punde, Bi Mtama akafariki dunia. Taswira ya kifo imetumika kutuonyesha kwamba maisha ya Semeni yanaongozwa na mivuto ambayo inamshinda nguvu na kamwe hawezi kuiongoza. Maisha ya Semeni yamepangwa kwa mujibu wa majaliwa.

Hatuna budi kusema kwamba Said Ahmed Mohamed ameathiriwa na mwelekeo wa falsafa ya kukata tamaa katika usawiri wa mhusika Semeni. Falsafa hii ya kukata tamaa imeendelezwa vizuri na mwandishi mashuhuri wa Algeria aitwaye Albert Camus (Cruickshank: 1958:27) anaposema:

> 'Maisha ya binadamu akiwa hapa duniani
> huwa yamepangwa kwa sababu za kimaumbile
> na kwa amri ya Mungu na hana analoweza
> kufanya kuyabadilisha' (tafsiri yetu)

Kwa kuthibiti dondoo hili, jukumu linalotekelezwa na jamaa katika malezi ya Semeni hatuonyeshwi. Baada ya mama kufa na baba kutoroka, jukumu la malezi lilichukuliwa na Shoga, Bi Mtama. Semeni amejaaliwa maisha ya adhabu.

Baada ya maisha pale mashambani kuwa magumu zaidi, Semeni aliamua kuingia mjini alikofikiria maisha yatakuwa afadhali:

> "Akaona labda mji, hwenda ukamwauni, hasa vile alivyowahi kuwasikia watu katika mazungumzo wakiusifu mji na kuupaka rangi rangi" (uk. 46).

Dondoo hili linatuonyesha kuwa Semeni amevutiwa na maisha ya mji. Kwa watu wasio na tajriba ya mji, maisha huwa danganyifu sana. Zaidi ya hayo, Semeni hana mtu wa kumtegemea huko mjini aendako. Bila shaka, sharti Semeni ataabike.

Semeni aingiapo mjini, mtu wa kwanza kukutana naye ni Binti Daudi. Mwandishi amemkutanisha Semeni na Binti Daudi ili kuendeleza falsafa yake inayotazama maisha kama adhabu. Tumetoa hoja hii kwa sababu Binti Daudi alitumika kama chombo cha kumnasia Mzee Zuberi Vigoli kama Semeni. Kwa muktadha huu, inaonekana kuwa makaribisho ya Semeni huko mjini yalikuwa ni tukio la hatari kwa maisha yake huku tukijua kwamba Semeni ni mnyonge wa nafsi na kiuchumi. Hana walezi, hana jamaa pia hana kazi.

Aila zisizo imara aghalabu huwapa watoto malezi yasiyo kamilifu. Malezi kama haya huwacha

ufa mkubwa katika maisha. Ufa huu huanzia na unyonge wa nafsi kisha unyonge wa kiuchumi hufuatia. Semeni ni mnyonge kweli kweli, hana mtu wa kumtegemea na hana njia yoyote ya kujipatia riziki.

Semeni aliwajibika kufanya kazi kwa Mzee Zuberi. Hata hivyo,Mzee Zuberi aliazimia kujinufaisha kutokana na unyonge wa Semeni:

> "Mjukuu wangu, unajivunjia riziki yako. ... kuna walionunuliwa nyumba mama, waliofuliwa vyombo vya dhahabu kochokocho... kuna wanaovaa na kubadili.... Bwana kama huyu kukutaka usimjamili! ... unajivunjia riziki zako we! (uk. 17)

Hivi vilikuwa viroja vyake Binti Daudi. Ijapokuwa Semeni alikuwa mhitaji wa kiuchumi alikataa katakata kubadilisha mwili wake kwa fedha. Ni katika sehemu hii ambapo tunaona msanii akiutetea utu wa Semeni. Semeni hakutaka kufanya kiunyume na imani yake.

Imani ya Semeni (uk. 46) ilikuwa ni kukaa na kumngojea mume wa kweli, mume wa ndoa. Jitihada zote hizi za Semeni kukataa mafedha hazikuweza kufua dafu kutokana na uafriti wa Mzee Zuberi aliyemnusisha dawa akiwa amelala na kumnajisi (uk. 11).

Msanii alishindwa kuendeleza ujasiri wa moyo wa Semeni. Kitendo cha uafriti alichofanyiwa na Zuberi kinatumika kama kigezo cha kuvunjika kwa ujasiri wake. Usawiri huu unadhihirisha hali ya kiyumbayumba. Said Ahmed Mohamed anayumbayumba kwa madhumuni ya kutimiza lengo lake; falsafa yake ni kwamba Semeni sharti ataabike mpaka siku ya mwisho. Hii ni kwa sababu mtu kuvunjiwa ubikira na kupewa mtoto haramu haina maana kwamba utu wake umetiliwa maji na ujasiri wa kupambana na ulimwengu kuyeyuka. Kuyeyuka kwa ujasiri ndiyo silaha ya msanii ya kutimiza falsafa yake ya majaliwa.

Baada ya semeni kutendewa unyama na Mzee Zuberi, alijiingiza mjini. Pale mjini ile nyota yake ya mateso inazidi kumwongoza. Anakutana na Pili ambaye alikuwa amejiingiza kwa maisha ya ukahaba. Makaribisho ya Pili kwa Semeni yalikuwa kama msumari wa moto:

> "Nitakaa na wewe ndugu yangu. Wewe una riziki yako na mimi nina nyangu". (uk. 47).

Kama tulivyotangulia kusema, falsfa ya mwandishi kuhusu maisha ya Semeni ni kwamba amejaaliwa maisha mbaya sana. Amezaliwa katika mateso na atakufa katika mateso. Hivyo, maisha yake ni ya kukatisha tamaa.

Semeni kukutana na Pili ni namna fulani ya kuendeleza majaaliwa. Hoja ya kwanza ni kwamba, Said Ahmed Mohamed anamwongoza Semeni katika mazingira mabaya kila wakati. Mashambani alishindwa na maisha hadi kiwango cha kuombaomba na kufedheheka. Pale kwa Mzee Zuberi alifedheheka zaidi kwa kunajisiwa na kutiwa himila. Zaidi ya hayo, anakutanishwa na Pili, aliyeishi maisha magumu ya kujinadi mabarabarani. Wa aidha, Semeni mgeni katika maisha ya mjini anaambiwa na mwenyeji wake aishi na kutegemea jasho lake. Kwa hakika, kokote Semeni aendako, makaribisho huwa ya kukatisha tamaa.

Nafsi ya Semeni inadhihirisha ujasiri wa kupambana na mambo ya kilimwengu, lakini mtu hawezi kupambana na kushinda majaaliwa:

> "Ingawa nyumba ile ilikuwa bohari ya laana na uchafu, alifumba macho kutia vizibo masikio siku nyingi, akaufanya moyo wake usitamani, hasa baada ya tendo alilotendwa na Zuberi (uk. 47).

Uhitaji ulimrahisisha na kupeana kile wanaume walichokichimba kwa siku nyingi. Wa aidha, mazingira alimoishi yalimvuta zaidi na kumwingiza katika ngoma ya ukahaba. Katika nyumba yao, palikuwa

na Pili, Riziki, Maulidi na Naima. Wote walishiriki ngoma ya ukahaba. Mazingira kama haya ni sawa na maradhi ya kuambukiza lazima kila mtu ayapate hayo maradhi hata awe na kinga kiasi kipi.

Msanii anawasawawiri watu wa mjini kama 'vifaa vya kuendeleza maovu'. Kila mtu aliyekutana na Semeni alimwingiza kwa maovu zaidi. Mathalani, Binti Daudi Zuberi na Pili. Hii si taswira yenye uhalisia kwamba watu wote waishio mijini ni maafriti. Usawiri huu wa Said Ahmed Mohamed umejitokeza tena katika Utengano, haswa katika usawiri wa Maimuna. Usawiri sawa na huu wa Said Ahmed Mohamed unaonekana kupitia kwa mhusika Rehema anayejitokeza katika kazi ya Mohamed Suleiman Mohamed iitwayo Nyota ya Rehema (1976).

Said Ahmed Mohamed hampatii mhusika Semeni nafasi na uhai wa kukua kifasihi. Semeni anauliwa mapema sana kiasi kwamba hatuwezi kutathmini fikira na falsafa yake kuhusiana na taasisi ya ukahaba na matatizo ya wanawake kwa jumla. Tena, kifo chake kinamdhalilisha sana kama binadamu. Binadamu anayejiua mwenyewe baada ya kuona maisha ni magumu ni binadamu ambaye hajakomaa kupambana na tesi za ulimwengu.

Kwa muhtasari, tunaweza kusema kwamba ukahaba wa Semeni ulisababishwa na ile hali ya kutokuwa na mihimili mizuri ya kifamilia pamoja na kutokuwa na tajriba ya mji. Hatuwezi kumlaumu sana Semeni, maana malezi yake na kukua kwake kulikuwa na doa. Doa hii ndiyo iliyosheheneza unyonge aliokuwa nao. Unyonge uliosababisha kifo chake hatimaye. Wa aidha unyonge wake ulizidishwa na ile hali ya kuzaa mtoto haramu, Chambilecho Little (1973:22).

> "Himila nje ya ndoa huleta fedheha na hudhalilisha nafsi... Wanaohusika huhisi ulimwengu umefika kikomo." (tafsiri yetu).

Hali ya mtu kufiwa na wazazi na kumpata mtoto haramu aghalabu huathiri maisha yake sana.

Mikondo ya maisha aliyopitia Semeni si tofauti na aliyopitia mhusika Wambui katika riwaya yake Mantago iitwayo <u>Trial of Jomo Kenyatta</u> (1970). Baada ya wazazi wa Wambui kufa, alitoroka Thika na kwenda Ol Kalau kuishi kama kahaba. Hata hivyo, sharti tufahamu kwamba maisha ya Semeni yanaongoza na nyota baya ya majaaliwa. Jitihada za ujasiri alizozifanya zilitosha kumwezesha kuishi maisha bora. Lakini yote aliyofanya yalikuwa sawa na'kupiga ngumi ukuta'

maana mtu hawezi kupambana na kushinda majaaliwa.

Pili, ni mhusika mwingine anayejitokeza hapa na pale katika Asali Chungu. Tumehamasishwa kuhakiki maisha ya Pili, Kwa vile ukahaba wake ulianzia wakati alipokuwa ameolewa na Bwana Shaabani Supu. Kama tulivyotangulia kusema katika sura ya Pili, kuna watu wengine ambao ni wachoyo sana. Uchoyo wa pesa una mapana na marefu yake. Hata hivyo, si wajibu wetu kutafiti chanzo cha uchoyo wa pesa katika tasnifu hii. La muhimu ni kwamba baadhi ya wanadamu huthamini pesa kuliko ndoa. Pili, akiwa mke wa mtu alikuwa akijiuza kwa matajiri wenye fedha haswa Waarabu kama vile Bopa, Bori na wengine.

Pili, alikuwa akiufanyia 'Uchafu' huu huko shamba. Baada ya kupewa talaka na mumewe, Pili, alikimbilia mjini na kuendelea kuuza mwili wake. Katika maelezo yake msanii, ametilia uzito mkubwa katika maisha ya Pili ya mjini kama kahaba na jinsi alivyoamua kurudi shamba kulima. Maelezo ya maisha ya Pili kabla ya kufika mjini tunayapata kupitia kwa mumewe. Ijapokuwa mumewe anaweza kuwa domo la msanii, undani wa maelezo hatuupati. Msanii ameyafungia macho maisha ya Pili ya mashambani.

Said Ahmed Mohamed ni msanii ambaye anahusisha, ukahaba na mazingira ya mjini. Wasanii wengine wenye msimamo kama Mohamed ni Cyprian Ekwensi katika riwaya zake People of the City (1954)na Jagua Nana (1961). Mawazo haya kwamba mashambani ni mazingira ya uadilifu na mjini ni mazingira ya ukahaba ni mawazo yasiyo na uhalisia.

Mohamed anataka tuamini kwamba talaka ndiyo uliyomfungilia Pili maisha ya ukahaba. Maisha aliyoishi ya kuzini nje ya ndoa kwa madhumuni ya pesa ni ukahaba wa wazi, kama asemavyo Little (1973:86)

> "Mapenzi nje ya ndoa ni hoja ya kawaida kwa maisha ya kisasa na aghalabu huleta pato kubwa kwa mwanamke anayehusika". (Tafsiri yetu).

Talaka yake Pili ilisababishwa na ukahaba wala si talaka iliyosababisha ukahaba. Tunachoweza kusema kuhusu kuhamia kwa Pili mjini na kuendelea na ukahaba wake ni kwamba labda hao wapenzi wake 'bandia' walishindwa kumkidhi kifedha pamoja na mtoto wake Baya. Tena, wanawake wengi hufikiria ukahaba unapato kubwa mjini kuliko ilivyo mashambani. Hoja ambayo ni kweli, maana mazingira ya mjini yana ulegevu wa kimaadili. Hivyo basi, mtu ana uhuru mkubwa sana wa kujinadi mabarabarani atakavyo.

Jambo moja la kusikitisha ni kuona kwamba msanii anambadilisha Pili, kimawazo anapokuwa mkongwe sana:

> Pili alihama mjini. Mji hautaki watu wakongwe, unataka vijana wenye nguvu... Tokea siku hiyo alibadilisha maisha. Alitaka riziki yake itoke mgongoni mwake, sio itoke kwenye mgongo wa mwanamume anayetaka kukidhiwa haja ya mara moja. Hivyo akakamatana na kiserema na ardhi akalima kuchumia tumbo. (uk. 183).

Mabadiliko ya Pili hatuwezi kuyathamini kama mabadiliko ya kimawazo. Mtu hubadilisha mawazo na kuchagua lipi la kutenda na lipi la kupuuza. Lakini mtu anapowajibika kufanya jambo fulani maana hakuna njia nyingine hatuafiki kama ni mabadiliko ya mawazo.

Pili ameamua kurudi mashambani kutokana na uzee na ile hali ya kukosa wateja. Hangeendelea kuishi mjini, kwa hivyo ilikuwa lazima kwake kurudi shamba. Isitoshe, hatuwezi kusema Pili amebadilisha maisha, labda tuseme amebadilisha mazingira. Uzee wake haumruhusu kujiingiza katika harakati ngumu za kujitafutia riziki. Alirudi shambani kusaidiwa na jamaa. 'Ngombe akivunjika guu malishoni hujikokota zizini kusaidiwa' kwa hivyo, msanii kumjaza Pili na lugha nzuri ya kubadilisha mawazo na maisha ni hoja isiyo na

mihimili.

Pili, amesawiriwa kama mhusika ambaye hana maisha nje ya ukahaba. Kule mashambani, alikuwa akiendeleza ukahaba sambamba na ndoa. Alipohamia mjini aliuendeleza ukahaba zaidi. Mhusika Pili, alipewa talaka mara mbili, talaka ya kwanza ilibatilishwa na akasamehewa. Lakini hakubadilisha tabia yake. Hii, inatufanya tuwaze je, Pili hangeishi vingine bila kusaliti nafsi yake katika mambo ya ukahaba. Labda, wana elimu-tabia wataeleza kuwa tabia ya Pili inadhihirisha kasoro katika kukua kwake, Freud Sigmund (1974).

Hali tunayoiona ya muwewe ya kuuza supu inatudhihirishia kwamba uchumi wake ni hafifu sana. Hivyo basi, inaonekana Pili alitumia ukahaba kustawisha uchumi wake. Kwa huu muktadha, taasisi ya ukahaba inatumika kutosheleza taasisi ya ndoa isiyoridhisha. Mawazo yanayoshabihiana na haya ya mhusika Pili yameendelezwa na mwana fasihi iitwaye Chesaina (1987). Chesaina (1987) anadai kwamba waandishi wengi hawatumii busara wanapowasawiri wanawake kama makahaba maana huwa wanafungia jicho hali yao ya kiuchumi. Anachojaribu kusema ni kuwa ni halali mwanamke kujiuza kama hali yake ya kichumi ni hafifu.

Hatuwezi kuyaafiki madai ya Chesaina (1987) kwa muktadha wa mhusika Pili. Kigezo kikuu cha ndoa ni uaminifu. Tutakuwa tukifanya kinyume cha matarajio ya jamii kama tutatumia kigezo cha kiuchumi kuhalalisha ukahaba kwa wanawake ambao wameolewa. Tunachoweza kusema kuhusu Pili ni kuwa yeye anathamini pesa kuliko ndoa, utu na mwili wake. Amesaliti nafsi yake na ya mumewe kwa sababu ya pesa.

Katika riwaya ya Utengano, tunahakiki maisha ya mhusika Maimuna na jinsi yalivyomwingiza katika hali ya kuuza mwili wake. Maimuna anatufungulia milango ya kuona jinsi utoro unavyoweza kumsukumia mtu katika maisha hatari na ya shida bila hiari yake.

Wasichana wengi hutorokea mijini kwa madhumuni ya kutafuta uhuru ambao wamenyimwa na wazazi au mabwana zao kama asemavyo Little (1973:22). Maimuna alitoroka kwao nyumbani kuepa maisha ya utawa aliyolazimishwa kuishi yeye na mamake. Hali ya utawa iliendelezwa sana katika mfumo wa kimwinyi. Kazi nyingi za kifasihi za kimwambao zenye kupata uhai wake kutokana na utamaduni wenye maadili ya Ki-islamu zimesheheneza hali ya utawa. Kazi ya awali zaidi ni yake Mwanakupona - Utenzi wa Mwanakupona (1958). Tutanukulu beti mbili kuhalalisha hoja hii:

Na ukitaka kutoka
Sharti rukhusa taka
Uonapo naudhika
Rudi kuikalia (Ubeti 44)

Fuata yake idhini
Awe radhi kwa yagini
Wala sikare ndiani
Saa yake ikaria (Ubeti 45).(Nabhany:1972).

Katika muktadha wa kimwinyi, mwanamke wa ki-Islamu alistahili kukaa ndani kwa muda mrefu. Kama ni hoja ya dharura ya kutoka nje, lazima apewe ruhusa na mumewe na muda wa kubaki nje uamuliwe na mume. Mume si lazima aruhusiwe na mke. Hali hii iliwanyima wanawake wengi uhuru wao wa kuitalii nchi yao. Wa aidha, itikadi hii iliwanyima wanawake nafasi ya kushiriki katika nyanja za uzalishaji mali.

Aghalabu, Mamwinyi walipendelea kuwatawisha wake na mabinti zao kwa madhumuni ya kujipatia nafasi ya uasherati. Mathalani, mhusika Maksuudi katika riwaya ya Utengano. Miongoni mwa kazi nyingine zinazoonyesha utawa ni yake Mohamed Said Abdalla iitwayo Mwana wa Yungi Hulewa (1976). Katika riwaya ya Mwana wa Yungi Hulewa sawa na Utengano, watawa wake waliweza kuvunja miiko ya utawa na kujitafutia uhuru wanaotaka.

Maimuna alikimbilia mjini kutafuta maisha yenye uhuru alionyimwa. Maimuna alitamani uhuru wa kutembea, uhuru wa mapenzi na uhuru wa kufanya kazi. Wasichana

wengine ambao wamekimbilia mijini na hatimaye kujikuta katika ukahaba kama Maimuna ni kama vile mhusika Rehema katika Nyota ya Rehema. Rehema alikimbilia mjini kutafuta maisha bora yasiyo na kunyanyaswa na mama wa kambo. Vile vile, katika riwaya hii ya Nyota ya Rehema, mhusika Kidawa alitoroka kuepa mume aliyemtesa. Naye Ruzuna alitoroka ugumu wa jembe. Katika riwaya yake Kiango iitwayo Jeraha la Moyo (1982), mhusika Mwamvita alitorokea mjini baada ya kupata himila. Katika riwaya ya Balisidya iitwayo Shida (1975) mhusika Matika alitorokea mjini kwenye anasa. Wote hawa walitumbukia katika ukahaba.

Maimuna alitaka uhuru wa kuingia na kutoka, uhuru wa kuchagua, uhuru wa mapenzi, uhuru wa kufanya kazi na kupata riziki kutokana na jasho lake (uk. 23). Uhuru Maimuna aliokuwa akiutafuta ni uhuru wa kuchezea maisha bila kuongozwa na wazazi. Wasichana wengi akiwepo Maimuna huwa hawana madhumuni maalum yanayowapeleka mijini. Kwa ujumla, huwa wanatamani zile starehe na anasa za kilimwengu. Wa aidha, wengi huwa hawana elimu na ujuzi wowote wa kazi. Zaidi ya hayo, wengi huwa hawana mtu wa kumtegemea pale mjini. Inakuwa ni vigumu sana kwa wasichana kama hawa kuyamudu maisha danganyifu ya mjini. Maisha ya ukahaba huwa ndiyo mwafaka kwao, maana hawana

mihimili yoyote ya kiuchumi.

Maimuna alihisi unyonge wa kunyimwa uhuru tofauti na wanawake wale wengine.

> "Akikumbuka huona maonevu, hasa akisoma na kusikia kwenye redio jinsi wanawake wenziwe wanavyopiga hatua katika maendeleo yao na maendeleo ya nchi zao" (Utengano, uk. 23).

Dondoo hili linatuonyesha jinsi Maimuna alivyokuwa na mawazo ya kutaka kujiendeleza pamoja na kuendeleza nchi yake. Lakini kikwanzo kikubwa ni wanaume wanao wanyanyasa kwa kuwatawishwa.

Kulingana na dondoo hili, msanii amezua hoja ya maendeleo ya wanawake. Hoja hii inaleta utata tunapoihusisha na dhamira ya mwandishi katika Utengano. Ijapokuwa si lazima mwandishi kuonyesha kila jambo, mtazamo wa mwandishi katika Utengano ni kuwa, wanawake hawajapewa nafasi ya maendeleo. Ni pale mwishoni mwa riwaya ndipo tunapoona wanawake wnaaanza kutambuliwa na serkali:

> "Serikali itafanya kampeni kubwa kuwaelimisha wanawake vijijini Maendeleo ya wanawake ni maendeleo ya jamii nzima, na ukombozi wa wanawake ni ukombozi wa jamii nzima (uk. 173).

Huu ndio ujumbe wa mwandishi kwa wanawake. Lakini tusisahau kwamba mwandishi naye ameipata itikadi hii kutoka kwa watangulizi wake, hususa wale wanamapinduzi wa Kiafrika Rais Kwame Nkrumah na Samora Machel. Samora Machel amenukuliwa na Mbilinyi (1983:34) akisema:

> "Mapinduzi yanayodhamiria kudumisha hadhi na maendeleo ya binadamu sharti yashirikishe ukombozi wa wanawake kutokana na unyanyasaji. Maendeleo ya jamii si maendeleo kitu ikiwa nafasi ya mwanamke itadharauliwa".

Mwandishi hakuweza kuhusisha vizuri itikadi yake na usawiri wake wa wahusika. Mwandishi anaposema Maimuna aliona maonevu aliposoma na kusikia redioni namna wanawake wanavyopiga hatua za kimaendeleo ni hoja ambayo hatuwezi kuiafiki. Suala kubwa ni je, Maimuna aliona maonevu baada ya kuona na kusoma maendeleo yepi? Katika riwaya zote nne za Said Ahmed Mohamed hatuoni mwanamke yeyote ambaye ameendelea. Wote ni duni. Labda maendeleo katika nchi nyingine.

Kwa hivyo, tunachoweza kusema ni kwamba msanii amemzaa, amemlea na kumkomaza Maimuna kabla ya wakati kuiva. Lugha ambayo msanii anamsawiri mhusika Maimuna nayo imemwinua sana kuliko jamii

anayotusawiria. Kumpeleka Maimuna katika maisha ya uhuru ili kupiga hatua ya kimaendeleo ni uzushi tu. Basi, kama ni kutetea utikadi yake, kwa nini anamwingiza katika ukahaba na hatimaye katika ndoa. Hizi zote ni taasisi zinazoendeleza ukandamizaji wa hali ya juu kulingana na jamii anayotusawiria.

Tashwishi nyingine kuhusu utoro wa Maimuna inaonekana kupitia kwa mapenzi aliyoyatamani. Maimuna alililia mapenzi, apendwe na apende anayetaka. Shida ni kwamba hatuoni vipi Maimuna angeyatamani mapenzi haswa baada ya kushuhudia mapenzi potovu na ya hatari ya Maksuudi na Tamina, wazazi wake. Isitoshe, katika mazingira yake hatuoni mapenzi yoyote ambayo yangepigiwa mifano. Wale 'maafriti' waliomsaidia kutoroka Binti Kocho na Farashuu walikuwa hawana mapenzi. Walikuwa hawana mabwana. Maimuna angejisaili na kuelewa ukweli wa maisha kabla ya kuchukua hatua hatari ya kutafuta mapenzi ilihali katika mazingira alimoishi kulikuwa hakuna hayo mapenzi. Kwa hivyo, msanii amemsawiri Maimuna kama duwazi. Mtu ambaye hawezi kujifunza kutokana na mazingira yake.

Maimuna aliweza kunaswa na maisha ya kilimwengu kwa urahisi kwa vile hakuwa na tajiriba ya maisha ya mji. Tena, Maimuna hakuwa na maandalizi yoyote.

Wale aliowafikiria marafiki zake, Farashuu na Binti Kocho walikuwa ni panya, ndiye huuma huku akipulizia.

Zaidi ya yote hayo, Maimuna hakutaka kujirahisisha kwa mwanamume yeyote:

> "Aling'ang'ania utu wake,
> kwani hakukimbia kwao kwa kuja
> kujiuza" (uk. 57).

Unyonge wa kiuchumi ulizidi kumwelemea kwa kukosa mhisani wa kumhudumia. Maimuna alilazimika kubadilisha imani yake na kuuchuuza mwili wake kwa yule aliyekuwa tayari kununua. Tena, tusisahau kwamba mazingira yalichangia sana katika kumfanya Maimuna kahaba. Alipotoroka kwao, alipelekwa kwa Mama Jeni. Mama Jeni aliendeleza biashara ya danguro. Kutoka hapo Maimuna alielekezwa kwa Binti Sururu. Hapa, biashara ilikuwa ya ukahaba na kuuza pombe. Kutokana na haya mazingira, ilikuwa ni lazima Maimuna 'kuambukizwa' ukahaba.

Uhuru Maimuna alioutaka hakuupata. Alikuja kutambua kwamba uhuru ni pesa:

> "... anaona kuolewa ni ndwele, ni
> kujifunga kwa mikataba bure. Kwake
> kubadilisha ndio maisha, ndio mchezo
> na ndio kazi, ndio pato. Hakuridhika
> tena na mmoja. Ilimbidi afanye kazi,

> kwa ajili ya pesa na kuishi. Wala hakukuwa na mapenzi. Mapenzi hayakuhusu. Pesa, pesa, pesa..." (uk. 87).

Mapenzi yaliyeyuka na badala yake akaanza kuthamini pesa. Baada ya kutambua thamani ya pesa, Maimuna aligeuka'mchovya asali ndiye hachovyi mara moja.'

Maisha ya Maimuna ya ukahaba yanasawiriwa katika jazanda ya ndoto inayojitokeza katika uk. 96:

> "...jinywa hili lilicheka na kumwitamwita Maimuna. Maimuna alikuwa anatetemeka. Naye akabanduka. Hatimaye, bila ya hiari alijiona ananyanyuka kutaka asitake. Akalisongelea lile jichwa la mende. Alipofika hapa, nyama lilifunua zaidi jinywa na Maimuna alitumbukia na jinywa likafumba. Nyama hilo halikutafuna, kwa hivyo Maimuna alielemea kwenye jinywa la Pili. Akaona atatoka nje. Lakini jinywa lilimkamata kwa ile mijino yake..."

Hii ndoto ya nduma kuwili lenye vinywa viwili katika kila ncha inaeleza jinsi Maimuna anavyokabiliwa na maisha hatari. Kinywa cha kwanza kinachekacheka kumwita, naye bila hiari anasongea na kutumbukia tumboni. Anajitahidi sana kutoka lakini jinywa la Pili linamkamata. Kinywa cha kwanza kuchekacheka kinadhihirisha jinsi maisha ya kilimwengu yanavyovutia, lakini baada ya kupandwa na anasa ni vigumu kujiokoa.

Isitoshe, jazanda hii inaonyesha kwamba jitihada zote za Maimuna zinamrudisha katika maisha yale yale ya ukahaba. Kutoka kwa Mama Jeni, kwenda kwa Binti Sururu na kadhalika.

Kwa mkururo huo huo, mwandishi anamwinua Maimuna kutoka ukahaba wa hali ya chini hadi ukahaba wa tabaka la juu kwa kumpeleka 'Rumbalola Hotel'. Vilabu vikubwa kama Rumbalola huwa ni mahali mwafaka kwa vipusa kujinadi kupitia kwa midemko na sauti zao za ninga. Dirasse (1978) anatueleza kuwa vipusa huweza kujipatia wateja wa tabaka la juu katika mazingira kama ya Rumbalola. Msichana mwingine ambaye ameinuliwa kutoka katika danguro na kupandishwa kiwango cha kuburudisha 'waungwana' kwa mdemko wake na sauti yake swafi ni mhusika Nana katika riwaya yake Zola iitwayo Nana.

Maimuna alijikuta katika ngoma ya ukahaba kutokana na unyonge wa nafsi uliosababishwa na hali ya utawa uliomnyima uhuru wake. Ni haki ya kila mtu kuufurahia uhuru wake. Hata hivyo, Maimuna alitoswa katika lindi hatari na marafiki zake aliowathamini watamsaidia. Kama si hawa 'maafriti' Binti Kocho na Farashuu labda tunaweza kusema kwamba Maimuna angeishi maisha bora zaidi, maana angejiandaa mwenyewe badala ya kuandaliwa ulimwengu na watu wenye ari ya kulipiza kisasi.

## 3.1.2. WAHUSIKA WANAOHUSIANA KWA MISINGI YA KIFEDHA AU FAIDA.

Katika sehemu ya 3.1.1. tumejadili jinsi wasichana wengi wamejikuta wakiuza miili yao bila hiari. Wengi wamefikia kiwango hiki baada ya kunaswa katika mikondo hatari ya kiuchumi.

Sehemu hii ya 3.1.2. inahusu uhakiki wa jinsi wahusika fulani wamesawiriwa wakihusiana, lakini uhusiano wao umejengeka katika misingi ya kufaidika kiuchumi au katika kukidhi nafsi yenye kiu ya tamaa za kimwili. Tutaweza kufikia malengo yetu kwa kunakidi uhusiano wa wahusika wafuatao:

<u>Asali Chungu</u>

Bi. Amina na Dude.

<u>Utengano</u>

Kazija, Maksuudi na Mussa.

<u>Dunia mtu mkavu</u>

Sakina na Inspekta Farouk

<u>Kiza katika Nuru</u>

Juba na Salma.

Katika Asali Chungu, mwandishi anaupinga sana utumwa wa kununuliwa kwa fedha kiasi kwamba mtu anasahau utu wake. Zuberi na mkewe Amina ndio watu ambao wanaamini kwamba fedha inaweza kuleta raha, fedha inaweza kununua mapenzi na kutawala watu ambao hawana fedha.

Bi. Amina alitumia uwezo wake wa kifedha kununua mapenzi kutoka kwa mabarubaru ambao wangeweza kukidhi uchu wake wa kimwili. Miongoni mwa wengine wengi, Amina aliweza kumnunua Dude na kuanzisha 'mapenzi' naye:

> "Kwa kweli si Dude tu, bali anatumia utajiri wake kuwa ni mtego wa kumnasia nobe yeyote ampe lile alilolihamu yeye" (uk. 103).

Haya ni maelezo ya utashi na ashiki ya Bi. Amina. Bi. Amina ni wale 'mashuga mami' wanaoandama vijana chipukizi wenye damu yenye nguvu kuzima ashiki yake. Kulingana na maelezo ya Bakwesegha (1982), wanawake kama hawa ni waenezi wakubwa wa ukahaba.

Kuna sababu mbalimbali ambazo labda ndizo zinamfanya Amina kujiingiza katika mapenzi ya kununua kwa pesa. Hoja ya kwanza ni kwamba, Amina mwenyewe alinunuliwa kwa pesa. Baada ya Mzee Zuberi kujiona mkubwa kwa umri kuliko Amina, alitupa pesa na kunasa

nobe wake; Amina.

Tukio hili, lilimfungulia Amina milango ya ukahaba maana aliamini kwamba hakuna mapenzi ya dhati. Mapenzi ni kuyanunua unapoyahitaji na mwenye kuuza ni mwenye njaa:

> "... toka lini mwenye njaa kapewa shibe akakataa? Kijana yule ana njaa. Akijua kuwa atakapotegemea ni pahala panono, mbona itakuwa rahisi kumteka". (uk. 62).

Kwa hivyo, imani ya Amina ni kwamba fedha ni raha na ni starehe. Amina hafahamu utu ni nini. Anafikiri kila mwenye njaa hana utu, mradi pesa. Amina aliweza kuwanasa malofa kama Dude wasiothamini utu. Hata hivyo, tufahamu kwamba Dude ni mhitaji na mhitaji ni mtumwa. Dude aliutetea utu wake hatimaye baada ya kuchuma.

Sababu nyingine ya Amina kununua mapenzi inaonekana kupitia kwa ile tabia ya uasherati ya matajiri wengi chambilecho Little (1973). Mamwinyi wengi aghalabu huwa na wapenzi wengi nje ya ndoa kama makahaba au masuria. Kutokana na hali hii wanawake wengi wameshindwa kuvumilia tabia hiyo ya kutokuwa na uaminifu. Hiyyo basi, wameamua kulipiza kisasi kwa waume zao. Isitoshe, wanawake wengine wanadai kwamba

kuishi na mume mmoja ni hali ya kuchosha sana kama asemavyo Little. (1973: 120):

> "Imani kwa mume ni hoja ya jadi na ni dhana ambayo imezikwa katika kaburi la sahau kwa wanawake wengi... Kuishi na mume mmoja ni hali ya kuchosha kwa wanawake wanaohisi damu yao ingali moto". (tafsiri yetu)

Si makosa kusema Amina analipisa kisasi kwa mumewe Zuberi, maana uzinzi ulikuwa ni nguzo katika maisha yake. Wa aidha, Amina inaamini kwamba damu yake ingali moto. Anadai kwamba mumewe ni Mzee sana na yeye bado chipukizi:

> 'Ah! labda si kosa langu, kwani Bwana Zuberi amenioa ningali mdogo sana; na pengine tofauti ya umri baina yetu unanifedhehesha". (uk. 61).

Kutokana na dondoo hili, tunaona kwamba msanii analaumu ndoa zinazofungwa kwa sababu ya pesa. Kama si pesa, Amina hangemkubali Mzee Zuberi kutokana na umri. Tena msanii analaumu sana ndoa zenye pengo kubwa la umri. Mapenzi ya dhati huweza kupatikana kwa watu wenye umri sawa au unaokaribiana. Hoja dhahiri hapa ni kuwa, makahaba hutekeleza jukumu la kutosheleza ndoa zisizoridhisha kwa sababu ya umri, ugonjwa na kadhalika.

Lakini hoja ya kusikitisha ni kuona kwamba Amina alijipatia nafasi hii ya kukimbizana na mabarubaru baada ya mumewe kupatwa na maradhi ya moyo. Badala ya Amina kukaa kitako na kumuuguza mumewe, alijipatia nafasi ya kustarehe nje. Amina ni mwanamke anayestahili lawama kwa kutomjali mumewe wakati wa maradhi. Hoja hii inadhihirisha ukweli wa msemo 'mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi'

Kwa mtazamo wa kisaikolojia, tunaweza kusema kuwa damu ya Amina ina chembechembe za uasherati. Nafsi yake ina unyonge wa kimapenzi. Kutokana na hali kuwa Amina aliolewa akiwa Chipukizi, labda alikuwa hajaonja 'asali', na ndiyo sasa inajitahidi kuchonga 'mzinga'.

Dude alilazimika kuuvunja utu na kuuza mwili wake kwa Amina kutokana na ulofa na unyonge wa kiuchumi:

> "Dude alinaswa kwa urahisi kutokana na ulofa wake pamoja na hali ngumu ya maisha yake toka kuzaliwa kwake".
> (uk. 104).

Dude alikuwa mhuni, mwizi ambaye alikuwa tayari ameishafungwa miaka miwili. Matatizo ya kiuchumi yaliyowakabili wasichana kama Maimuna, Dora, kijakazi

na Semeni hadi kiwango cha kuuza miili yao si tofauti na yale yaliyompata Dude. Hivyo, aliwajibika kuuza mwili wake kwa walio tayari kununua kama Amina.

Kama tulivyosema katika Sura ya Pili, uhusiano wa makahaba hauna udhati wa kimapenzi:

> "Fadhila ni utumwa ilikuwa ni vigumu kwake kumvunja Bi. Amina, kwani ingawa hakuwa na mapenzi na bibi huyu, alikuwa na shukrani kubwa kwa msaada wake". (uk. 118).

Mwili wa Dude ulinunuliwa na Bi. Amina kwa bei nafuu:

> "Nenda kwa Mahendra, Bwana Dude akachaguwe suti tano atakazo. Bili akupe uniletee. (uk. 96).

Dude kupitia uhusiano wake na Amina alinufaika kwa mavazi, fedha, kazi na hata akaweza kujipatia gari la kusafiria.

Dude baada ya kuchuma atakavyo unyonge unamwondokea:

> "Dude hataki tena kufa, anataka kuishi, kuishi ni haki ya viumbe. Kujiua ni kujidhulumu. Mauti aliyoyataka zamani, ... unyonge ameshausahau". (uk. 118).

Hoja inayojitokeza waziwazi ni kwamba baada ya unyonge kuondoka utu hurejea tena. Utu ulimrejea Dude na akaanza kuona kwamba Bi. Amina anamlemeza na kumpotosha. Mwandishi natumia jazanda ya nyota kumzindua Dude:

> "Mimi ni nyota ovu, nimekuja badala ya nyota yako njema. Nimekuja kukwambia kuwa dunia hii si yako, usiiamini". (uk. 132).

Nyota imetumika katika ndoto hii kwa maana ya utabiri. Elimu ya nyota hutumika kueleza bahati ya mtu ya siku zijazo. Dude kuonywa asiamini dunia ni njia nyingine ya kuonywa dhidi ya kujifanya mtumwa wa pesa kwa kuudunisha utu wake. Dude alipokaa, aliweza kusikia sauti dhaifu:

> "Na wewe, hata wewe Dude! wewe si mtu kumbe Wewe si mwanaume. Umeharibiwa, umenunuliwa na mwanamke huyo. Wewe umeolewa. Wewe mtumwa". (uk. 131-2).

Asili ya maneno haya yalitoka katika kinywa cha mhusika Baya (uk. 127). Mwandishi alimtumia mtu duni kama Baya kumzindua Dude. Baya anatumika kama domo la msanii kumzindua Dude kabla maisha yake hayajapotoshwa na Bi. Amina. Hata hivyo kuzinduka kwake kuna walakini:

> "Majuto, majuto sina, nina wasiwasi tu kukosa yale mapesa yake..." (uk. 134).

Ama kwa hakika, mwandishi amegeuza mawazo ya Dude kisebusebu tu. Dude yungali anatawaliwa na pesa. Alijitenga na Bi. Amina kwa kuogopa fedheha kutoka kwa marafiki zake. Kama si kuogopa fedheha, Dude angeendelea kuchuma zaidi. Ili atimize matarajio ya wengine, Dude alianza kutafuta mke halisi wa ndoa. Hata hivyo, 'Mchovya asali hachovyi mara moja.' Dude aliendelea na uasherati hadi akatia doa ndoa yake kwa kumtia himila Latifa, dadake Shemsha, mke wake.

> "Dunia Mti Mkavu ya S.A. Mohamed kufikia sasa inawakilisha kilele cha maendeleo ya riwaya ya Kiswahili katika

> uchanganuzi wake wa kisiasa na kijamii kuhusu mabadiliko ya upembuzi wa jamii za Kiafrika (Mazrui: 1984:9). (tafsiri yetu).

Kama riwaya zile nyingine, S.A. Mohamed katika Dunia Mti Mkavu amefaulu katika kusawiri wahusika wake kuwakilisha makundi mbalimbali katika jamii, wakiwepo, watamba-na-njia, mafalahi, watumishi, wafanyakazi wa mashambani na mijini, mamwinyi na mabepari, Njogu (1987:3). Katika riwaya hii, tunaazimia kujishughulisha na kipengee maalumu ambacho hakijajitokeza katika riwaya zile nyingine isipokuwa katika Kiza katika Nuru. Hiki ni kipengee kinachohusu uhusiano wa kikazi baina ya mwajiri na mwajiriwa.

Mbilinyi (1983:22-23) ametafiti kuhusu uhusiano wa kazini na ametambulisha kuwa wanawake na wanaume wengi wamebabaishwa sana hadi kufikia kiwango cha kuuza miili yao na kutoa hongo ndipo waweze kupata kazi. Hamu ya kutaka kazi ili kujiepusha na unyonge wa kuombaomba au kutamba na njia ndiyo imemfanya mhusika Sakina kuutupilia mbali utu na kuusalamisha mwili wake kwa Insipekta Farouk ndipo aweze kupata kazi ya uhazili.

Tumepitia kazi kemkemu za fasihi zinazotusawiria wasichana wengi walioahidiwa kazi kwa masharti fulani:

> 'Kupeana ni kikoa, toa nawe upewe.
> Bila ya hivyo hakuna kazi'.
> (Dunia Mti Mkavu)(uk. 84).

Haya ni maneno ya Insipekta Farouk akimwambia Sakina. Sakina kwa msukumo wa uhitaji hana lingine ila kukubali kuuza mwili wake ndipo apate kazi:

> "... Nitafanyaje na mimi ni mhitaji"
> (uk. 84).

Sakina ni mnyonge na mnyonge hana haki. Sakina hana hiari maana anataka kujihimili katika maisha. Mwandishi anatupatia taswira ya kisasa ambapo wanawake wanataka kujitenga kutoka kwa minyororo ya kumtegemea mwanamume kiuchumi. Hata hivyo, huku kujitegemea kuna vikwazo kutokana na uafriti wa maofisa fulani.

Katika Kiza Katika Nuru, Salma, mhazili wa Juba aliwajibika kuacha kazi maana hakutaka kudhalilisha nafsi yake kwa kuuza mwili wake kwa bosi wake Juba. Juba alimshawishi Salma kwa ahadi za kumwongeza mshahara na kumpandisha cheo kazini, lakini Salma alikataa katakata. Hatimaye, Juba alimwachisha kazi Salma. Salma ni kiwakilishi cha wasichana ambao wana utu imara, utu usioyumbayumba. Ni kupitia kwa ujasiri kama wa Salma ndipo wasichana au wanawake wengi wataweza kuhifadhi utu na nafsi zao. Salma atabaki msichana wa kupigiwa mifano

maana baada ya kuachishwa kazi hakujiingiza katika mambo ya anasa na ukahaba, badala yake alienda shamba kulima na hatimaye kuolewa. Mwandishi alijaribu kumwepusha Salma na maisha ya mji, maana itikadi yake ni kwamba mji ni hatari sana kwa wasichana kama Salma. Salma ni kiwakilishi cha mwandishi anayetaka kuwatetea wanawake.

Usawiri wa mhusika Sakina katika Dunia Mti Mkavu unashabihiana sana na usawiri wa mhusika Mwamvita katika Jeraha la Moyo. Baada ya Mwamvita kutiwa himila akiwa chuoni, alikimbilia mjini alipokutana na maofisa wadanganyifu na wenye uchu kama Insipketa Farouk. Baada ya wanaume kufanikiwa katika matakwa yao, walimpiga mateke Mwamvita. Mwamvita alilazimika kujinadi mabarabarani na kurahisisha nafsi yake huku akijua kwamba 'ukikipata kitumie, ukikikosa kijutie'.

Mwandishi anawashtumu 'mabwana' kama Insipekta Farouk ambao hawathamini haki. Farouk haoni thamani ya binadamu wenzake badala yake anawaona kama vyombo vya kustarehesha. Farouk haonyeshi kuthamini umuhimu wa Sakina kama mfanyikazi katika ofisi yake. Angethamini umuhimu wa Sakina pale ofisini basi hangehitaji huduma za kimwili. Nafsi ya Farouk imelemazwa na unyonge wa

kutaka hongo. Falsafa ya Farouk na wengine kama yeye inaweza kuelezeka kwa maneno haya ya Ekwensi (1954:40-41):

> 'Hongo ni sawa na ukahaba, hujulikana na anayetoa na anayepokea, hakuna mtu ambaye huumia, basi kwa nini kujali?.... Karani, msichana mwenye sura nzuri, akirahisisha nafsi yake na kutoa mwili wake, mtamwona tajiri baada ya miaka mitano tu'. (Tafsiri yetu).

Dondoo hili linatuonyesha jinsi watu fulani wanavyojali kuridhisha nafsi zao badala ya kujali utu wa yule wanayemdhulumu. Hii ni hali ya kukosekana kwa hisia za kibinadamu.

Ukweli ni kuwa Said Ahmed Mohamed ametusawiria wahusika fulani wasio na hisia za kibinadamu, kutokana na utashi na ashiki. Inspekta Farouk ni mmoja wao kufuatia mjadala wetu na ziada ni kwamba aliweza kubatilisha kesi ya bwana Suleiman kama alikuwa tayari kupeana binti yake, Lulua, kwa Inspekta Farouk:

> '... Nampenda Lulua, ... kwa ajili yake nitafanya lolote; nitasimama kubatilisha haki.' (uk. 80).

Katika <u>Asali Chungu</u>, tunaona unyama wa aina hii pale ambapo mzee Zuberi alikuwa tayari kumsamehe Mzee Omari deni lake kama atakubali bintiye Mboga apeane

mwili wake kwa Zuberi:

> 'Iko njia moja ambayo itakuokoa
> na yote hayo... Leo usiku namtaka
> Mboga awe mgeni wangu'. (uk. 19).

Japo Mzee Omari ni Mzee anayestahili heshima na hadhi yake, Zuberi hakuona aibu kabisa kumwambia Mzee huyo akamlete binti yake ili aweze kusamehewa deni lake. Zuberi anaamini wazi kwamba kwa vile Omari hana fedha za kulipa deni, atafanya kila njia amuuze binti yake. Azimio hili la Zuberi na Farouk ni dhihirisho la kukosa utu na kujawa na unyama, hali ambayo chanzo chake ni ubinafsi.

Katika ukurasa wa kwanza wa riwaya ya Utengano tunakumbana na mhusika Kazija. Kazija tunaelezwa ni kipusa cha kutia wanaume mbioni. Kutokana na urembo wake, Kazija ni chombo cha kujiuza bila kunadi. Wasichana kama Kazija sawa na Jagua Nana katika riwaya ya Ekwensi Jagua Nana wanaamini kwamba, ' kwa vile Maulana hakuwatunuka mali, amewatunuka urembo. Kwa hivyo, wana imani kuwa ni mapenzi ya Mungu mtu kutumia alichotunukiwa:

> "Mwone Kazija, bibi mrembo anayejua
> vilivyo kungarisha uso, kutia wanja,
> kutimua shore... halafu uje utazame
> kanzu zinavyomchukua, zote maji yake...

> Ukaja ulaghai wa macho yake na tena ulimi wake wa kulazia, upole wa tabia yake... na zaidi jamala ya sura yake". (uk. I).

Upembuzi wa kinafsia wa huyu mwanamke Kazija unatudhihirisha moja kwa moja kwamba yeye hujipamba kwa madhumuni ya kuwanasa wanaume. Hisia zake zinamwelekeza katika imani kwamba mwanamke ni chombo cha kuuza. Hivyo basi, bei yake inategemea wingi wa madoido.

Tangu enzi za umwinyi na ubepari, wanawake wamekuwa mbioni kwa mashindano ya kuwanasa wanaume kama asemavyo Reed (1970:78). Katika jamii hizi za matabaka mwanamke alidunishwa kiwango kwamba lazima amtegemee mwanamume kiuchumi. Kutokana na hali hii, wanawake walilazimika kujikwatua ndipo wanase wanaume matajiri.

Kujikwatua kwa Kazija kulimwezesha kuchuma kutoka kwa Bwana Maksuudi. Maksuudi tumjuavyo si kidogo, aliwahi kuwa mwanzilishi wa Chama cha Waafrika, akawa mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Shirika la Bima la Taifa. Kwa muktadha huu, Kazija ni kielelezo cha ukahaba wa tabaka la juu. Makahaba wa tabaka la juu hujikwatua kwa madhumuni ya kunasa

watumishi wakubwa wa serikali, wanasiasa, wana falsafa na kadhalika:

> 'Mla nyama ya nguruwe, huchagua aliyenona... lazima ahakikishe mchumo wake. (uk. 3).

Kazija si kama mhusika kijakazi ambaye anamwendea Shoka kwa shillingi zake tatu (uk. 110). Wanawake kama Kazija huwachagua wapenzi wao kwa ungalifu mkubwa wasije wakapoteza hadhi yao:

> "Babu we! hutanitia mikononi halafu uniache ni fedheheke". (uk. 4).

Haya ni maneno ya Kazija kwa Mussa, mwanawe Maksuudi. Ijapokuwa Mussa hakuwa amefikia kiwango cha Kazija, Kazija alimkubali kwa minajili ya kutekeleza njama yake na Farashuu:

> "Baadaye, Kazija alitambua kwamba alikuwa na sababu kubwa ya kumkubali Mussa... Mussa alikuwa mtoto wa Maksuudi..... Kazija alikuwa na deni alilotaka kumlipa bwana huyu kwa ajili ya Shoga yake Farashuu". (uk.5).

Dondoo hili linatuonyesha vile mapenzi ya kuchuuza huweza kutumiwa kama silaha ya kuhujumu.

Usawiri huu wa mhusika Kazija wa Said Ahmed Mohamed unashabihiana na usawiri wa baadhi ya wahusika wa Mohamed Suleiman Mohamed katika Nyota ya Rehema na David Mailu katika Unfit for Human Consumption (1973). Wasanii hawa wana itikadi kwamba wasichana wanaoishi maisha ya ukahaba ni viumbe viovu vinavyoleta michafuko katika jamii; aila kutengana, watu kupigana au kujiua.

Mohamed Suleiman Mohamed anawatumia wahusika wake kidawa, Ruzuna na Chiku kulipiza kisasi kwa wanaume maana waliwatesa katika ndoa zao (Nyota ya Rehema, uk. 44). Vivyo hivyo, Kazija anatumika kama fimbo ya kumwadhibu Maksuudi kutokana na vile alivyomtenda mwana Sururu Bintiye Farashuu
Mailu anamtumia Lily, kumgonganisha kinama na mkewe, Dorcas. Aghalabu, usawiri kama huu hupotosha ule ubinadamu kiasi kwamba tungedhani makahaba ni maafriti wasio na hisia za kibinadamu. Hata hivyo, mtazamo wa Sigmund Freud (1976) ni kuwa makahaba hutumia 'mapenzi' yao kulipiza kisasi kwa wanaume ambao wamewanyima mapenzi ya dhati tangu utotoni.

Maelezo ya huyu mwana saikolojia yanaafikiana na maelezo yake Mama Jeni kwa Maimuna alipomwambia:

> 'Watose, ndio watose; maana sisi tumeshatoswa'. (Utengano, uk. 68).

Hali hii inaonyesha kwamba, makahaba huwatesa wanaume kwa kuwaibia na kuwafumanisha maana wanaamini kuwa mwanamume ndiye kisababishi cha maisha yao ya ukahaba.

Mapingano ya Maksuudi na Mussa ni kama ushindi wa medali kwa Kazija:

> 'Kazija alikufa kwa kicheko. Alicheka mpaka machozi yakamtiririka'. (uk. 15).

Kicheko kwa muktadha huu, ni tamathali ya Semi na mbinu ya kifani ambayo msanii anaitumia kutusawiria udhaifu wa mapenzi ya kununua. Uhusiano wa Kazija na Maksuudi umejengeka katika misingi ya mapato. Hii ndiyo sababu Kazija yuko tayari kumusubu Maksuudi hadharani (uk. 86).

Mwandishi amemsawiri Kazija akihusiana na ofisa wa Serikali, Maksuudi , kwa makusudi ya kuonyesha ufisadi na upotovu wa kimaadili katika jamii nzima. Kwa hivyo, mwandishi anamhusisha mwanamke wa maadili potovu na kiongozi kwa minajili ya kushtumu uozo wa jamii kwa jumla. Waandishi wengine ambao wamefanya sawa na

Said Ahmed Mohamed ni Kezilahabi katika Rosa Mistika, Aluko katika Chief the Honourable Minsiter (1970) pamoja na Singh Katika Sweet Schum of Freedom (1968). Waandishi wote hawa wamewahusisha makahaba na viongozi wa serikali. Ujumbe wa waandishi hawa kwa wasomaji ni kuwa viongozi wamepuuza wajibu wao. Wanatumia vyeo vyao na uwezo wao wa kifedha kuwapotosha wanyonge. Ili ni dhihirisha kuwa kila mtu katika jamii ni mshiriki mkubwa katika kuendeleza taasisi ya ukahaba.

Usawiri wa Kazija unatuonyesha kwamba yeye ameamua kuishi 'maisha huru' na maisha ya kujitegemea. Kazija amefanya hivi ili kujiepusha na taasisi za ukandamizaji. Taasisi ya kwanza ya ukandamizaji wa wanawake ni ndoa. Ndoa zote zinazojitokeza katika Utengano zinakandamiza wanawake. Labda hii ndiyo sababu ilimfanya Kazija kuamua kutoolewa hata chuo kimoja (uk. 4). Pia, angeamua kujishughulisha na maisha ya viwandani au ofisini, angekandamizwa zaidi na mabepari wanaotaka kuridhisha nafsi zao zenye kiu. Mathalani, mhusika Sakina anavyofanyiwa katika Dunia Mti Mkavu. Wa aidha, Kazija ameamua kushirikiana na mabepari na mamwinyi wanaowakandamiza wanyonge. Kile mamwinyi wanachochuma kwa haramu kutoka kwa makabwela, Kazija ana nafasi yake.

> '... Dunia hii hayendi bila pesa... Unapopata nafasi ya 'kula kula! na mwanamke mwepesi wa kuliwa'. (uk. 12).

Kazija ana nafasi kubwa kutoka kwa mchumo wa Maksuudi. Ukahaba wa tabaka la juu ni namna fulani ya kubadilisha mwili kwa zawadi lakini si papo hapo.

Mwandishi ameshindwa kumsawiri na kumweka mhusika Kazija katika nafasi yake mwafaka ya kijamii na kiuchumi. Mwandishi anamjaza mhusika Kazija na maneno mengi yanayodhihirisha unyonge wake wa kijamii na kiuchumi. Hata hivyo, unyonge wake haujitokezi katika maisha yake tunayosawiriwa. Kwa hivyo, inatufanya tuwaona Kazija wawili, Kazija mnyonge katika fikira na Kazija ambaye si mnyonge katika maisha. Labda, tuseme unyonge wake ni kielelezo cha unyonge wa wanawake kwa jumla katika riwaya ya Utengano. Na hwenda ndiyo sababu ametokea mwanzoni mwa riwaya na kusema maneno mazito ya ukombozi na kupotea. Hii inatuonyesha kwamba Kazija ni kipaza sauti cha msanii. Hatuwezi kumpima kwa maneno yake maana ni mtetezi wa tabaka duni kwa jumla.

Kwa kutathmini maisha wanamoishi hawa wahusika ambao tumewajadili, tunaona kwamba wanaishi maisha ya kupigana vita. Vita baina ya wanyonge na wasio

wanyonge. Wasio na pesa wanataka kuishi na wenye pesa wanataka kuwatumia bure. Basi, inakuwa ni vita baina ya mnyonge na ulimwengu wake. Ulimwengu ambao umejaa kila namna ya uovu; ubinafsi, unafiki, ukandamizaji, tadi na kadhalika.

Kila mhusika anatoa chembe chembe zake za unyonge. Unyonge wa kufiwa au kutengwa na wazazi, unyonge wa kunyimwa uhuru na unyonge wa kichumi. Kazija katika <u>Utengano</u> analalamika kuhusu unyonge wa kutosoma na unyonge wa kujipamba kwa madhumuni ya kumfurahisha mwanamume ambaye ndiye tegemeo lake la kiuchumi.

Kwa kunakidi hisia za hawa wahusika, tunapata wazo kwamba hakuna yeyote anayefurahia kunadi mwili kwa madhumuni ya kuchuma. Mazingira hatari na magumu ya kiuchumi ndiyo yamewafanya wazirahisishe nafsi zao na kutupilia mbali utu. Utu ni nini mbele ya kifo? Hatari ya kuangamia huweza kulainisha roho hata iwe ngumu kama mwamba. Shida na madhila hubadilisha imani. Jambo lililoonekana baya hapo awali huonekana zuri hatimaye. Makahaba wote walibadilishwa na uhitaji. Roho zao zikalainika, wakasalimu amri na kutoa lile ambalo watu wamekuwa wakilichimba.

## SURA YA NNE

### 4.0. JINSI MWANDISHI ANAWAONDOSHA WAHUSIKA WAKE KUTOKA KWA MAISHA YA UKAHABA

Mwandishi huzaa viumbe vyake na kuviacha vikue kimawazo, kijamii, kisiasa na kadhalika. Kukua huku ndiko kunawafanya wahusika wengi kubadilisha mtazamo wao wa kimaisha. Twafahamu kwamba wahusika ni heba ya mwandishi. Wahusika ndio hutoa mawazo na ujumbe wa mwandishi. Kwa hivyo,mabadiliko na matendo yote ya mhusika ni kwa mujibu wa matakwa ya mwandishi chambilecho Mohamed (1984:40):

> "Wahusika wangu hawahurumia mfano wa watoto wangu. Huwapenda wafanyapo matendo ya kuridhisha yanayokubalika na wengi katika jamii yangu. Huwachukia pale wanapofanya kinyume na utu wa ubinadamu".

Ni kwa mtazamo wa dondoo hili ndiyo sababu waandishi wengi wa fasihi ya Kiafrika wana mtindo wa kuwasawiri wahusika wabaya mwanzoni na hatimaye wanageuzwa kuwa wema zaidi.

Said Ahmed Mohamed anajishughulisha na lile swala la kuwepo kwa mwanadamu. Mwanadamu ni lazima aishi, lakini inasikitisha kwamba maisha yake mara nyingi hayawezi kuwa mazuri kwani tayari yameishatiwa dosari na wana-jamii wenzake

ambao wamekwishaharibiwa na jamii mbovu.

Said Ahmed Mohamed mara nyingi huwahurumia sana wahusika wake. Hataki wahusika wake waishi maisha mabaya daima-dawamu. Anajaribu sana kuwaokoa kutokana na maisha ya kizakwa kuwaonyesha maisha yenye utu. Maisha yanolenga mafanikio kwa siku za usoni.

Mhusika mwenye ujasiri wa kupambana na tesi za ulimwengu huwa na nafasi kubwa ya kubadilisha maisha yake magumu kuwa rahisi kama asemavyo Teyie (1982:8). Said Ahmed Mohamed anawapa baadhi ya wahusika wake wanaoishi maisha ya kujiuza nafasi ya kubadilisha mawazo. Baadhi ya wahusika wamebadilisha mawazo yao na wamehamia mashambani kulima. Wengine wameamua kujiunga na taasisi ya ndoa.

Hali hii inatudhihirishia kwamba, binadamu ana uwezo wa kubadilisha maisha yake kutoka hali anayoiona baya hadi kwa hali anayofikiria ni nzuri. Mabadiliko kama haya hudhihirisha uhalisia wa maisha, chambilecho Gikandi (1979:8):

> 'Uhalisia ni hali ya kuelewa
> misukosuko katika jamii zetu
> na kutambulisha mbinu tunazoweza
> kutumia katika kuyakwepa masuala
> magumu yanayoleta madhila na
> vikwazo katika maendeleo
> yetu' (tafsiri yetu).

Mtu anapoamua kuachana na ukahaba na kuingia katika taasisi ya ndoa au kushikamana na kiserema kulima ni namna fulani ya kuanzisha sura mpya ya maisha. Lakini hatuwezi kusema moja kwa moja, kuwa hizi sura mpya za maisha zitaleta maendeleo mazuri. Mathalani, taasisi ya ndoa imekuwa ikiendeleza ukandamizaji unaoshabihiana na ukahaba.

Katika kukabiliana na maisha magumu ya ukahaba, mwandishi anapendekeza kwamba mwanadamu anaweza kujiua kama suluhisho la kukwepa hali ngumu ya maisha. Baadhi ya madhumuni ya sura hii ya tasnifu, ni kutathmini matumizi ya kifo katika kuelezea hali ya jamii. Kifo, haswa mtu kujiua ni suala la umuhimu mkubwa katika fasihi maana sharti kuelezea falsafa ya mwandishi.

Hoja nyingine ambazo zitajadiliwa katika sura hii ni dhima na nafasi inayotekelezwa na taasisi ya ndoa kama suluhisho la ukahaba. Pia, tutajadili uhusiano uliopo kati ya mazingira ya mashambani na yale ya mjini katika kuchangia kuwepo kwa ukahaba. Suala tunalojadili hapa ni kwa nini Said Ahmed Mohamed anawabadilisha baadhi ya wahusika wake makahaba kwa kuwahamisha kutoka mjini hadi mashambani.

## 4.1. MATUMIZI YA KIFO KATIKA FASIHI

Katika kazi za fasihi, tunakumbana na aina mbili kuu ya vifo. Kwanza,kuna kile kifo cha mhusika kukata roho. Mhusika anaweza kukata roho kwa kuuliwa na watu wengine au kujiiua mwenyewe. Kifo cha pili ni kile tunachokiita kifo cha kisanaa. Kifo cha kisanaa ni kile ambacho mhusika hutoweka katika mfululizo wa visa bila maelezo kamili.

Said Ahmed Mohamed ametumia aina yote ya vifo katika riwaya zake. Mhusika kazija katika Utengano anapatwa na kifo cha kisanaa. Kazija ameendelezwa vizuri sana katika sura ya kwanza ya riwaya ya Utengano. Hata hivyo, kazija anatoweka bila maelezo yoyote kutoka kwa mwandishi. Hatutahakiki kifo cha kisanaa cha mhusika kazija kwa sababu uhakiki wake hautatusaidia kufikia malengo ya sura hii ya tasnifu. Madhumuni yetu katika sura hii ni kuhakiki namna ambavyo Said Ahmed Mohamed anayabadilisha maisha ya wahusika wake makahaba.

Kifo cha kukata roho katika wahusika makahaba wa Said Ahmed Mohamed kimetokea kwa mhusika Semeni katika riwaya ya Asali Chungu. Mhusika

Semeni alijiua baada ya kulemewa na mzigo wa maisha. Mtu hujiua baada ya kushindwa kuvumilia fujo za ulimwengu. Kifo kama hiki huweza kutumulikia kuona maonevu mengi katika jamii.

Said Ahmed Mohamed, miongoni mwa waandishi wengi anatumia kifo kama suluhisho kwa baadhi ya wahusika wake walio katika madhila. Waandishi wengine ambao wako katika mkondo wa kutumia kifo kwa madhumuni ya kuwaondoa wahusika katika maisha magumu ni kama vile Euphrase kazilahabi katika riwaya ya Rosa Mistika. Kezilahabi anamwondoshea matatizo mhusika wake Rosa kwa kifo. Mohamed Suleiman Mohamed katika kiu alifanya vivyo hivyo kwa mhusika Bahati. Ngugi wa Thiong'o katika riwaya iitwayo Petals of Blood alitumia kifo kumaliza matatizo ya mhusika Wanja.

Wahusika hawa wote ambao tumewataja waliishi kama makahaba. Mhusika Semeni katika Asali Chungu amesawiriwa kwa mwelekeo wa falsafa ya kukata tamaa. Falsafa ya kukata tamaa ni imani kwamba dunia ni mahali pabaya au mambo yote yaelekea uovu, Kaufmann (1976:239).

Mwandishi mwenye mwelekeo wa falsafa ya kukata tamaa huonyesha kwamba mwanadamu hana uwezo wa kubadilisha hali yake na kuifanya kuwa bora zaidi. Wa aidha, maisha ya binadamu ni kifo cha polepole na kaburi huwa hatua ya mwisho, Kezilahabi (1974:206).

> "Ukweli ni kwamba sisi wanadamu tunakufa polepole, watu wengi wanafikiri kwamba kifo kinakuja mara moja. Hili ni jambo la uwongo. Tangu mwanadamu anapo-zaliwa anaanza kufa polepole ingawa yeye anajiona sawa".

Said Ahmed Mohamed inaonekana ameathiriwa na falsafa hii ya kukata tamaa katika kumsawiri mhusika Semeni. Semeni tangu kuzaliwa hadi kufa ameishi maisha mabaya sana.

Mwandishi mashuhuri wa Algeria aiitwaye Albert Camus, Cruickshank 1958:40) na Mwanafalsafa wa Jadi Socrates (Gibbs:1968:2) wanasema kwamba ni haki ya mtu kujiiua ili kujiepusha na maisha magumu. Wana-elimu nafsia, wanadai kwamba mtu uamua kujiiua anapokataliwa na jamii. Wa aidha, mtu anapokosa mapenzi na mihimili yoyote katika jamii, ni kawaida kujiiua maana kwake maisha hayana ladha, Gibbs (1968:10). Mwana-elimu jamii, Emile Durkheim katika kitabu chake, Suicide: A Study in Sociology (1957)

anasema kuwa watu wengi hujiua katika jamii zinazosheheneza ubinafsi na tadi. Anaendelea kusema kwamba katika jamii hizi, kila mtu hujitahidi kivyake kuendeleza maisha yake na anaposhindwa, aghalabu kifo ndicho suluhisho.

Fasihi ni taasisi inayojumlisha taaluma nyingi. Mwandishi wa fasihi ni mwanasaikolojia, mwanasosholojia na mwanafalsafa wa jamii yake. Mwandishi ana jukumu la kufunza kuelimisha, kukanya, kuzindua, kushtumu na kadhalika, Palmer (1979:9).

Kifo kama suluhisho la maisha ni suala la mjadala sana, Chambilecho Chacha (1985:105). Mwanafasihi Chacha (1985), anamsimamo kwamba kifo hakistahili kutumika kama suluhisho, badala yake jamii inastahili kuelimishwa kuhusu shida zinazowakabili wana jamii wake. Huu ni mtizamo wa kijuu juu sana. Mtazamo ambao unaliangalia suala la kifo kama suala la mtu binafsi bila kuangalia umuhimu wake katika kuibua uozo na maonevu mengi ambayo yamefichika katika jamii.

Chacha (1985) anaendelea kusema kwamba watu kama mhusika Rosa katika riwaya ya Kezilahabi Rosa Mistika, ambao tayari wameishapakwa uvundo na jamii iliyooza hawana nafasi katika jamii. Inastahili wafe kabla ya

kuolewa na kuzaana. Hatuafiki falsafa hii ya Chacha (1985), maana kama tutatatua matatizo katika jamii kwa kuwaondoa waliopakwa uvundo, ni sawa na kuondoa kumbikumbi na kuacha mabuu. Wale waliokwisha pakwa uvundo katika jamii hawana hatari yoyote na kuwaangamiza ni bure maana wenye kupakana uvundo wapo na wataendelea kuwapaka wengine wengi. 'Mti hukatwa mizizini siyo shinani'. Maana yake ni kuwa, kuwaondoa watu kama mhusika Rosa na kuwaacha Deogratias, Bwana Maendeleo ya mwanzo, na mwalimu mkuu wa Morogoro T.T.C. si suluhisho lolote. Hawa mabwana wataendelea kuwapotosha wasichana wengine wengi. Falsafa ya Said Ahmed Mohamed ni mwafaka, maana anawaua Zuberi, Bi. Amina, Binti Daudi katika Asali Chungu, Maksuudi katika Utengano na Juba katika Kiza katika Nuru. Watu hawa ndio chanzo cha uozo wa jamii.

Semeni katika Asali Chungu, kama Rosa wa Kezilahabi katika Rosa Mistika alijiiua. Kujiua mbali na kuonekana kama njia ya kukwepa mazingira magumu ya kijamii ni njia mwafaka ya kushtumu maonevu yote yanayoendelea katika jamii hiyo. Yaani ni afadhali kifo kuliko kuendelea kuishi katika hiyo jamii. Semeni anathamini kifo kuliko maisha katika jamii alimoishi.

Taswira ya kifo cha Semeni kama binadamu ni taswira ya kifo cha jamii yote. Jamii ambayo imeshindwa kutekeleza wajibu wake. Wajibu wa kutosheleza matakwa ya wana-jamii wake. Taasisi zote za jamii zimeshindwa kutekeleza jukumu lake. Ubinafsi umeifanya jamii kuoza. Hivyo, jamii yote imekufa na twajua kwamba kufa kwa kinywa, mate hutawanyika'.

Jamii inaposheheneza mitafaruku na ubinafsi, watu hawawezi kuungana pamoja kwa madhumuni ya maendeleo, Gibbs (1968:23). Jamii ambayo Said Ahmed Mohamed anatusawiria ni jamii ambayo kila mtu yuko mbioni kuridhisha nafsi yake bila kujali matokeo yake kwa wengine. Aghalabu, kila taasisi inapokosa kupeana mwongozo mwafaka, wanajamii huanza kukata tamaa.

Taasisi ya familia imepuuza wajibu wake. Familia ya Semeni imetengana. Kifo kimemtenga Mama. Baba amejitenga na kutorokea kusikojulikana. Semeni ameachiwa mbuyu atafune na huku hana meno. Kutoroka kwa baba kunaonyesha ile hali ya mtu kuasi wajibu wake katika jamii. Kulingana na Mckee (1965:445) familia humfunza mtoto jinsi ya kukaa katika jamii na jinsi anavyoweza kutumikia jamii yake.

Viongozi ambao wanatarajiwa kuiongoza jamii vizuri wamepuuza wajibu wao. Viongozi huwa kama wazazi wa watoto katika jamii. Kwa muktadha wa Semeni wale ambao wangemwongoza walimpotosha kabisa. Mathalani, Mzee Zuberi. Zuberi kama Mkuu wa Wilaya na tena kama mzazi angemwonyesha Semeni njia nzuri ya kufuata badala ya kumfanyia unyama kwa kumnajisi na kutomshughulikia baada ya kumtia himila. Binti Daudi kama Mama mzee anastahili kumpatia mtoto Semeni mawaidha mazuri badala ya kumpotosha kwa vishawishi vya pesa kutoka kwa Mzee Zuberi.

Taasisi ya ushoga inasheheneza uchoyo na ubinafsi. Hii inadhihirika kupitia kwa ushoga wa Semeni na Pili:

> "Pili, alikuwa katoka, kamwacha Semeni, 'kalala kitandani, anaumwa. Akamwambia, "Akija mgeni wangu, mwambie aningojee; nakuja sasa hivi'. Mgeni akaja, lakini kwanza alikaribishwa na kukirimiwa na Semeni. Kwa bahati huku nyuma akatokea Pili, akazifumania kayaya zile. Yote Semeni aliyomtendea Pili, hilo haikustahamilika.... Kisha akamwambia kuwa siku ya Pili ingekuwa bora ahame nyumbani mwake. Asubuhi ilipofika, Semeni alihama kweli. Hakuhama nyumbani mwa pili tu, bali aliihama dunia; akakutwa kanyoka mkavu kitandani pake. Aliuacha ulimwengu uliojifunga kumtesa". (uk.48).

Semeni alijua kwa muktadha wa kufumuniwa akifanya mapenzi na rafiki wa mwenzie. Hii ina udhihirishia jinsi jamii imechafuka na imekuwa ni uwanja wa fujo. Kitendo Semeni alichomfanyia shoga yake Pili hakifai. Kitendo hiki kinatuonyesha jinsi pesa na ubinafsi umeharibu uhusiano wa binadmu. Ubinafsi hutia watu kiwi kiasi kwamba hawawezi kupata suluhisho la matatizo yao. Semeni alifikiria kifo ndio mwafaka kama suluhisho la maisha ambayo yanaonekana kama adhabu.

Semeni hana familia ya kumhudumia, jamaa hawapo, hakuna shoga wa kumsaidia na jamii kwa jumla inamtesa. Ni lipi tena la kutegemea? Hata baada ya kujirahisisha na kujinadi mabarabarani, maisha yalimtumbukia nyongo:

> "UjanaJike wake ukafikia kileleni; akawa anashindwa kuhesabu pato lake la kutwa sikwambii la kucha. Fedha zikaingia mikononi mwake kama zinavyo-ingia mikononi mwa karani wa benki. ... Mpanda ngazi kushuka, na wa kileleni kamungojee Shinani. Akaanza kuporomoka. Taratibu wanaume wakaanza kumkinai; mwishowe, akapuuzwa ... Damu ikampungua; akawa hana damu namna ya jongoo. Akili pia ikawa inapungua kila siku. (uk. 48).

Kazi ya Semeni ya kujitolea mhanga na kuutupa utu ilikosa wateja. Hivyo basi, mapambano ya wanyonge ya kujiendeleza aghalabu hukatisha tamaa sana na matumaini kwao ni nadra na hafifu sana. Hatari ni kwamba, kama

wanyonge watakata tamaa kama Semeni, itawachukua muda mrefu sana kupambana na kushinda matatizo yanayowakabili katika jamii.

Tunaposoma kazi ya fasihi, huwa tunachukua jukumu la jamii ambayo imeandikiwa. Wasomaji ndio jamii. Athari tunazopata ndizo mwandishi huwa amedhamiria kufikia jamii. Mwandishi anapotusawiria maisha ya kusikitisha kama ya Semeni, anataka tujione kama ndio tuliosababisha kifo cha Semeni. Anataka kila mtu aone makosa yake na afikirie jinsi angeyazuia yote hayo kutendeka. Sisi kama wazazi, marafiki na hata viongozi ndio tumesababisha kifo cha Semeni. Ili wanyonge waone thamani ya maisha, ni lazima jamii ibadilishe mifumo na maadili yake kwa minajili ya wanyonge walio wengi.

## 4.2. KUHAMIA MAZINGIRA YA MASHAMBANI.

> "Fasihi nyingi za Kiafrika zimezua taharuki kuhusiana na jukumu linalotekelezwa na maisha ya mjini ukilinganisha na yale ya mashambani katika kutusawiria uhusiano wa binadamu na jamii yake".
> (Mutiso: 1974:73)
> (Tafsiri yetu).

Dondoo hili linalenga kumulika mikinzano inayoibuka kuhusiana na mazingira haya tofauti; mazingira ya mjini na ya mashambani. Ijapokuwa ni kweli kwamba mazingira ya mjini yameathiriwa sana na anasa za kimagharibi kama vile sinema, ulevi wa marika yote, 'mapenzi huru' na kadhalika, wasanii wengi wameyapaka rangi nzuri mazingira ya mashambani. Hizi rangi rangi ambazo zimepakwa mazingira ya mashambani zinatufanya tuwaze je, jamii za mashambani hazibadiliki?

Waandishi wengi wa Kiafrika akiwemo Saidi Ahmed Mohamed wamefaulu sana katika kuwasawiri wahusika wao na ule uhai wa kifasihi unaowawezesha kubadilisha maisha yao. Mabadiliko makuu yanayojitokeza ni yale ya kutoka katika uovu na kuingia katika wema. Mabadiliko haya mara nyingi huenda sambamba na mabadiliko ya kimazingira. Kuna itikadi ya waandishi ya kuhusisha ubaya na mazingira ya miji ilihali wema unahusishwa na mazingira ya mashambani. Kwa kutathmini mazingira haya tofauti, tunaona mwanya mkubwa kiasi kwamba hatuwezi kuafiki yote ni mazingira katika jamii moja. Mawazo kama haya yanaendelezwa sana na Raymond (1975:9) anaposema:

> 'Mashambani ni mazingira ya amani, uaminifu na uadilifu. Mjini ni mahali pa misukosuko, uhuni na mambo mengi ya kilimwengu (tafsisi yetu).

Kwa hivyo, imekuwa ni itikadi ya waandishi wengi kuwa mabadiliko na uzuri wa mtu (mhusika) unaweza kudhihirika chini ya mazingira ya mashambani. Maisha ya shamba huonekana kuwa ni shwari, mazuri na ambayo hayajaingiliwa na athari za kigeni, chambilecho Kezilahabi (1971:84).

> "Ukimwuliza mtu wa shamba habari kuhusu maisha yake atakwambia. 'Maisha ya shamba ndugu yangu ni mazuri. Huwa ni baridi. Ubaridi huu unakifanya kichwa kufikiri bila kelele. Hakuna vumbi, majani kila mahali na miti yenye maua mazuri hupendeza macho!" (uk. 84).

Dondoo hili latuonyesha vile waandishi wanavyoyaona maisha ya mashambani kuwa ni mazuri kwa kiasi fulani na yasiyokuwa na dosa.

Waandishi wengi wa fasihi ya Kiafrika hutumia mbinu ya kuwarejesha mashambani wahusika ambao wanakuwa wakiishi maisha 'machafu' na magumu mijini. Wahusika hawa ni kama vile makahaba, wezi na wengine. Falsafa ya waandishi hawa ni kuwa, kurejea mashambani ni njia mwafaka ya kusuluhisha baadhi ya matatizo yao ya kiuchumi. Hoja hii ina utata sana maana kumrudisha mtu mashambani labda si kusuluhisha matatizo yake lakini ni kuhamisha matatizo hayo katika mazingira mapya.

Said Ahmed Mohamed amewarejesha baadhi ya wahusika wake mashambani baada ya mapambano magumu ya kujiuza pale mjini. Mhusika Maimuna katika Utengano baada ya kuishi maisha ya kung'ang'ania wanaume katika vilabu alirejea shamba huko Futoni na kuolewa na kabi. Mhusika Pili katika Asali Chungu pia alirejea mashambani baada ya maisha sawa na ya Maimuna ya kujiuza. Mhusika Dude baada ya kuwa mwizi pamoja na kujiuza kwa wanawake wenye mali kama Bi. Amina alirejea shamba huko Kisauni.

Kama tulivyotangulia kusema, usawiri kama huu umeendelezwa na waandishi wengi: Mohamed Suleiman Mohamed katika Nyota ya Rehema amemsawiri mhusika Rehema sawa na Maimuna wa Said Ahmed Mohamed. Rehema baada ya kukimbizana na maisha ya mjini huku akijiuza kwa kujinadi mabarabarani, aliweza kubadili mwenendo na kurudi mashambani na kuolewa na Sulubu. Katika riwaya yake May Lenna Ndyanao Balisidya iitwayo Shida, Mhusika Matika alijinadi kila pembe katika barabara na vilabu vya mji wa Dar-es-Salaam. Hatimaye, aling'amua upungufu wa maisha ya mji na kurudi shamba Dodoma na kuolewa. Mhusika Jagua Nana katika riwaya ya Cyprian Ekwensi Jagua Nana, alijitumbukiza katika anasa, ukahaba na uasherati katika mji wa Lagos na hatimaye nyota ilimwongoza kurudi mashambani. Usawiri kama huu umeendelezwa na waandishi wengine wengi.

Wahusika wote wa Said Ahmed Mohamed wanaoishi katika mazingira ya mjini wanatupatia sifa za kukosa ubinadamu, utu na maadili mema, tofauti na anavyotusawiria maisha ya mashambani. Hatuna budi kusema kuwa falsafa ya Said Ahmed Mohamed ni ya kututahadharisha kuhusu maisha ya miji. Hii inadhihirika kutokana na namna anavyoyapaka mazingira ya mashambani rangi rangile:

> 'Maimuna aliukimbia mji wa Bobea kwa kitambo cha meli arubaini. Akahamia shamba, Futoni, Pahala palipokuwa na utaratibu mkubwa na upole kwa binadamu. (Utengano, uk. 148).

Kuhusu maisha ya Dude na mkewe, Shemsha , ya shamba, mwandishi ana haya ya kusema:

> 'Mara nyingine walipita vichakani kutazama uzuri wa mimea, maua, matunda na ndege'. (Asali Chungu, uk. 160).

Dondoo hizi zinatuonyesha ile hali ya utulivu wa mazingira ya mashambani. Hoja inayojitokeza hapa ni kwamba wote wanaoishi mashambani wametosheka na hawana usumbufu wowote.

Huko mashambani, mwandishi anawasawiri wahusika wake kwa lugha inayodhihirisha utulivu na mandhari

yanayovutia ukilinganisha na mazingira ya mjini:

> 'Sasa Maimuna alijihusudu mwenyewe. Jinsi alivyopata mwili na siha. Mwili wake ulirejesha hali yake ya uzima. Kivimbo chake kilimrejea, akatakata. Damu ilimwiva na nguvu na siha zilikubali kushirikiana naye tena'. (Utengano, uk. 172).

Lugha inayotumika kumsawiri Maimuna na mazingira yake inaonyesha hali ya raha. Hali isiyo na unyonge. Hali inayoonyesha kutosheka na maisha. Afya ya mtu ni kigezo muhimu sana cha kupimia hali yake ya uzima kama tunavyoona katika dondoo hili. Tukilinganisha na hali yake ya kiafya hapo mbeleni alipong'ang'ania uhuru huko mjini, Maimuma amestawi sana.

Licha ya hayo, mwandishi anatusawiria mandhari na mazingira yanayovutia.

> 'Ikiwa mtu anaelekea mlangoni kwao, anakutana na muhogo uliostawi na migomba mingi, ya mkono wa tembo, mzuzu, pukusa na ntwike. Hii imepandwa kwa safu na nafasi baina yao imeipa kunawiri... Konde zote hizo ni za nyumbani tu, mbali na zile walizonazo bondeni'. (Utengano, uk. 171).

Kustawi kwa konde hizi ni taswira inayotumulikia kuona kustawi kwa Maimuna katika maisha yake mapya ya mashambani. Kwa upande wa mhusika Pili katika

Asali Chungu, mwandishi anatusawiria hali yake ya kufurahia maisha mapya aliyokuwa akiishi pale mashambani:

> '... Alikamatana na Kiserema na ardhi... aliridhika nayo kuliko yale ya mjini ya kutegema riziki inayotoka mikononi mwa watu wengine'. (uk. 184).

Kurudi kwa Maimuna mashambani kunadhihirisha kushindwa kwa falsafa yake kwamba uhuru hupatikana mjini. Isitoshe, kurudi kwa Maimuna kunatudhihirishia kushindwa kwa usasa na desturi za jadi kupata nguvu. Fikira za Maimuna kuhusu maisha ya kisasa haziambatani na misingi ya wazazi wake (baba), hata ingawa misingi hii imejikita katika utamaduni mkongwe unaohitaji kubadilishwa ili watu waweze kuendelea. Hii ni kutokana na hoja kwamba Maimuna alitoroka kwao kujiepusha na maisha ya utawa. Katika jamii nyingi za kiupwa zilizoongozwa na maadili ya dini ya Kiislamu, wanawake kutawishwa ilikuwa ni desturi.

Mwandishi ameshindwa kuendeleza dhamira yake katika usawiri wa mhusika Maimuna. Amekanganya ujumbe wake. Dhamira kuu ilikuwa ni kuwatetea wahusika wake wa kike, ndio sababu akamtorosha Maimuna kutoka katika maisha ya utawa; maana kutawisha wanawake ni hoja ya kuwahini haki ya kuishi kama watu huru; tena utawa ni

amri na miko inayozuia ukamilifu na maendeleo ya mtu.

Baada ya kuvunja miko ya utawa, Maimuna anakuwa huru kutenda atakavyo pasina kuamrishwa. Uhuru wa Maimuna una uchachu sana. Uhuru wake hausaidii kuinua hadhi yake bali unamfanya kudidimia zaidi. Uhuru wa Maimuna wa kuzama katika lindi la ukahaba unakatisha tamaa sana. Mwandishi ameshindwa kuendeleza uhuru wa Maimuna; badala yake anamrudisha mashambani na kumwingiza katika taasisi inayoendeleza ukandamizaji na uonevu kwa wanawake. Nayo ni taasisi ya ndoa.

Mwandishi amemrejesha Maimuna shamba ili kushtumu ile dhana ya vijana wengi wa siku hizi wanaoamini kwamba uhuru ni anasa; kucheza densi, kufanya mapenzi na mambo mengine mengi ya kilimwengu. Isitoshe, mwandishi anatuonyesha kwamba hizi ni taathira za kimagharibi. Lazima tutafute uhuru wetu katika mazingira yetu mwafaka bila kukimbilia uhuru mjini. Ujumbe wa mwandishi ni kuwa maisha ya mijini hayana furaha bali ni mateso, hofu, fujo na kadhalika. Furaha inaweza kupatikana katika maisha ya mashambani. Hii ndiyo sababu wengi wanaoasi na kukimbilia mijini hatimaye hurudi nyumbani. Mathalani, mhusika Jagua Nana katika riwaya ya Ekwensi <u>Jagua Nana</u>, mhusika Matika katika riwaya ya Balisidya iitwayo <u>Shida</u>.

Lakini si kweli, kusema kuwa maisha ya mashambani hayana vituko na vitimbi. Michafuko iko kila mahali lakini kwa kiasi fulani, maisha ya shamba ni tulivu kidogo.

Mzunguko wa maisha ya Maimuna hadi kurudi mashambani si tofauti na yaliyotokea kwa maisha ya mhusika Pili katika Asali Chungu. Sawa na vile Maimuna hakuridhika na maisha ya utawa, ndivyo Pili hakurudhishwa na maisha ya ndoa yake na Shaabani Supu. Ile hali ya kutoridhisha nafsi ndiyo iliyomfanya amwendee mumewe kinyume. Alifanya hivyo kwa mujibu wa kutosheleza nafsi yake na labda hali yake ya kiuchumi. Pili alitaka kuyafanya maisha yake bora zaidi, lakini uhuru alioutaka wa kimapenzi hauwezi kupatikana katika ndoa. Hii ndiyo sababu akapewa talaka. Baada ya talaka, alikimbilia mjini alikofikiria kuna nafasi kubwa ya uhuru wa kuchagua na kubadilisha wanaume aliwathamini.

Matamanio ya Pili hayakuweza kutimizika maana jamii haiwezi kuyaafiki mambo aliyoyatamani sawa na maisha aliyoyataka Maimuna. Uhuru wa kuchezea mapenzi na anasa nyingine ni upotuvu kwa mtazamo wa jamii nyingi za Kiafrika. Hivyo basi, mwandishi anawaongoza wahusika wake katika maisha mwafaka na yenye maadili na mafunzo

yanayokubaliwa na jamii-mpya anayoipendekeza.

Wahakiki wengi wamewashtumu waandishi wanaowasawiria wahusika wao katika hali ya masikitiko kutoka mwanzo hadi mwisho. Mathalani, Teyie (1982:8) anashtumu Meja Mwangi kwa kukosa kipengee cha maendeleo katika wahusika wake wanaotamba na njia katika riwaya zake Kill Me Quick (1978), Going Down River Road (1976) na The Cockroach Dance (1979). Teyie anaendelea kusema kuwa Mhusika huonyesha uhalisia zaidi kama atapatiwa nafasi ya kubadilisha maisha yake.

Aghalabu,maendeleo na mabadiliko fulani yanayopatiwa baadhi ya wahusika katika kazi za fasihi si maendeleo kamwe bali ni visingizio tu. Said Ahmed Mohamed kumrudisha Maimuna mashambani hatuwezi kusema ni mabadiliko ya kimaendeleo. Anachofanya mwandishi ni kumwondosha katika uhalisia ili atimize ule uhai wa kifasihi. Maisha aliyopitia Maimuna pale mjini ni hali halisia. Maisha ya ukahaba, maisha ya kuabudu pesa na maisha ya ubinafsi yamejaa kila mahali na si kweli kwamba mazingira ya mashambani ni yale yale ya kijadi ambayo hayajafikiwa na hizi taathira za kimagharibi. Kwa hivyo, mwandishi anawabadilisha wahusika katika jamii ambayo haibadiliki kwa kiasi fulani.

Falsafa hii ya mwandishi kwa kiasi fulani inasingizia mazingira maovu fulani. Anaonyesha kuwa kama si kwa mazingira ya mji labda mambo fulani kama ukahaba hayangendeka. Tutasingizia mazingira mpaka lini? Ingefaa zaidi na ingekuwa hali halisi kama wahusika kama Maimuna na wengine wangebadilishwa katika mazingira yale yale ya mjini. Waandishi wanastahili kutafuta mbinu nyingine za kuwabadilisha wahusika kuliko kuwapeleka mashambani. Uadilifu na utaratibu tunaohadithiwa kuhusu mazingira ya mashambani ni hali ya kijadi na haupo kabisa kwa maisha tuyoshuhudia leo hii.

Itikadi ya kurejea mashambani siyo mpya hapa Afrika Mashariki. Baada ya uhuru, wanasiasa wengi walianza kuwahimiza wale waliokuwa hawana kazi mijini kama makahaba na wengine kurudi mashambani kulima, Bakwesegha (1982). Waandishi na wanasiasa wamekuwa wakiwasisitiza watamba-na-njia kurudi mashambani. Hii ni hoja ya kusikitisha maana watamba-na-njia ndio wanaorudishwa shamba. Ukweli ni kwamba, hii ni fikira ya kikoloni kwamba miji ni mahali mwafaka kwa watu wa tabaka la juu ilihali shamba ni mwafaka kwa watu wa tabaka la chini.

Kwa mtazamo wa kiuchumi, mwandishi amemrudisha Maimuna, Dude na Pili shamba ili kututahadharisha kuhusu ugumu wa kiuchumi katika miji mingi. Marx na Engels katika Selected Work Vol. III (1966) wanadai kwamba maisha ya viwandani ndiyo yaliyozua kipengee cha pesa. Kipengee ambacho kilimtia kitanzi binadamu wa tabaka la chini. Maisha ya viwandani yaliathiri jamii zilizoishi kwa muundo wa kitamaduni Watu walianza kuuza mazao yao ya kilimo kwa minajili pesa. Wengine walianza kuhamia mijini kwa matumaini ya kuajiriwa wapate pesa. Wengi waliokosa kazi viwandani walianza kuuza miili yao, wengine wakawa wevi na kadhalika.

Mfumo wote huu uliuvunja utu na ubinadamu. Hoja inayojitokeza kutokana na riwaya za Said Ahmed Mohamed ni kwamba pesa ambazo ndizo kiini cha ubinafsi na kuvunjika kwa utu wa binadamu ziliwaathiri watu wa mijini na kuacha watu wa shamba:

> 'Hutaki - hutaki pesa? aliuliza Maimuna kwa wasiwasi. pesa? Nini pesa mbele ya utu? (Utengano, uk. 161).

Haya majibizano ya Maimuna na Kabi yanatuonyesha kwamba watu wa shamba (Kabi) hawajaguswa na mfumo wa kuabudu pesa. Hii ni itikadi ambayo imeshikiliwa na watu wengi

kwamba wasichana au wavulana wazuri wa kuoa au kuolewa wako shamba, hoja ambayo haiwezi kuwa ni kweli.

Onyo la mwandishi kwa wasomaji ni kwamba miji imetawaliwa na nyanja za kiuchumi zinazosheheneza ukandamizaji na ubinafsi kutokana na athari za maisha ya viwandani ya kuabudu pesa. Tunapokimbilia mijini kwa matumaini ya kujiendeleza kiuchumi ni sawa na kujitosa katika lindi la maonevu na mateso. Bora tujiimarishe kwa uchumi wetu wa kilimo ambao haujaingiliwa sana na ukandamizaji. Uchumi wenye ushirika kama inavyodhihirika katika maisha mapya ya Maimuna na Kabi, Dude na Shemsha.

Kwa mtazamo huo huo, anachofanya mwandishi ni kujaribu kupendekeza au kuunda jamii mpya yenye fikira mpya. Hii jamii mpya itakuwa ni jamii ya wakulima na wafanyikazi ambao wataishi kwa kusaidiana kutoa mchango mkubwa kwa taifa lao changa. Inaonekana Said Ahmed Mohamed ameathiriwa na mfumo wa nchi yake wa ujamaa. Mfumo unaopendekeza ushirika wa wakulima, Mbilinyi (1983). Lakini jamii kama hii anayopendekeza ni ya kukisia tu. Sharti jamii ya kilimo iathiriwe na maisha ya viwandani maana wakulima watawajibika kuuza mazao yao kwa minajili ya pesa. Isitoshe, haiwezekani jamii yote kujishughulisha katika kilimo, lazima pawe na

makarani, makuli na hata wafanyikazi katika majumba ya anasa. Watu kama hawa hawawezi kukwepa taathira za maisha ya viwandani. Wa aidha, katika majumba haya watu kama Maimuna, Dude, Pili na Semeni sharti wawe wengi sana.

## 4.3. TAASISI YA NDOA

Riwaya nyingi za Kiswahili hujihusisha na wasichana na wavulana waliopotoka. Licha ya hayo, baadhi ya waandishi wameonyesha wazi kwamba upotovu ni hali ambayo mtu anaweza kuikwepa. Mtu yeyote yule anaweza kuepukana na maisha yasiyoafikiana na maadili ya jamii.

Fasihi ni taaluma inayojumlisha taasisi nyingi za jamii. Mathalani, ndoa, ukahaba, siasa na kadhalika. Wajibu wa fasihi ni kumulika ili wasomaji waelewe jinsi taasisi mbalimbali zinavyowiana na jinsi uwiano huo unyavyolingana na uhalisia wa maisha, Lowry (1974).

Tumejadili kwa marefu na mapana taasisi ya ukahaba katika tasnifu hii. Sehemu hii (4.3) imetengwa kujadili taasisi ya ndoa na vile inavyolandana na taasisi ya ukahaba. Wa aidha, tutatizama jinsi Said Ahmed Mohamed anatusawiria taasisi ya ndoa kama suluhisho ya taasisi ya ukahaba.

Ndoa na ukahaba hujengeka katika misingi sawa ya mapenzi, lakini miktadha yake hutofautiana. Ndoa inastahili kuwa na mapenzi ya dhati ilhali ukahaba una mapenzi ya kununua kwa pesa au zawadi. Ni kawaida kwamba watu fulani hujiunga na ukahaba punde tu ndoa zao zinapovunjika. Vivyo hivyo, ukahaba ukileta nuksi watu wengine hukimbilia katika ndoa.

Baada ya ndoa ya Pili na Shaabani Supu katika riwaya ya Asali Chungu kupata janga, Pili alikimbilia ukahaba. Mhusika Chiku katika Nyota ya Rehema aliposhindwa kuvumilia uasherati wa mumewe, alijitosa katika ukahaba. Maimuna katika Utengano baada ya kutambua hakuna matumaini mazuri katika maisha ya ukahaba, aliamua kuolewa, ndoa ambayo hakuithamini hapa mbeleni:

> '... anaona kuolewa ni ndwele, ni kujifunga kwa mikataba bure. Kwake kubadilisha ndio maisha, ndio mchezo, ndio kazi na ndio pato' (uk. 87).

Maelezo haya yanatuonyesha namna ambavyo taasisi ya ukahaba na ndoa huchangiana.

Itikadi ya Said Ahmed Mohamed ni kutetea walio wengi, nao ni wanyonge. Hii ndiyo sababu anatusawiria jamii ambayo wanyonge wako katika harakati za

kujiendeleza. Wanyonge wanaonekana wakisaidiana wenyewe kwa wenyewe. Hii ni ishara kuwa mwandishi ni 'mkombozi' wa wanyonge.

Wanyonge wengi wameweza kuzisahau shida zao na kujitahidi wawezavyo kuwasaidia wengine watoke kwenye shimo la dhiki. Mathalani, Baya katika Asali Chungu ndiye 'Mwokozi' wa Dude:

> 'Na wewe, hata wewe Dude!
> wewe si mtu kumbe.
> si mwanamume. Umeharibiwa,
> umenunuliwa na mwanamke huyu.
> Wewe umeolewa. Wewe mtumwa.
> (uk. 121).

Baya ni msichana aliyekuwa akiishi maisha sawa na Dude na labda ya Dude ni afadhali. Baya aliweza kuona hatari ya kuangamia kwa Dude ndipo akamzindua Hatari iliyomkabili Dude ni hatari inayoangamiza vijana wengi wa siku hizi ambao hawana fahamu ya siku zijazo. Hatari ya kununuliwa na 'Mashuga mami'.

Kwa kurejelea riwaya ya Utengano, tunaona hali ya Maimuna ikishabihiana na ile ya Dude. Baada ya maisha ya Maimuna kuharibika kabisa, ndipo Kabi alipojitokeza na kumwokoa kwa kumwoa. Kabi ni mnyonge zaidi, kwanza ni kilema, Pili alitegemea kolekole na vidagaa wanaoachwa katika upwa na maji ya bahari.

Mifano kemkemu ya ndoa za 'ukombozi' kama za Maimuna na Dude zimejitokeza kwengineko katika utanzu wa riwaya za Kiswahili. Rehema katika Nyota ya Rehema alijisalimisha kwa mnyonge mwenzake Sulubu na kuoana baada ya harakati za kujiuza hapa na pale. Mhusika Matika katika Shida aliokolewa na kijana mwenzake aliyekuwa mwizi maarufu katika mji wa Dar-es-Salaam.

Lerner (1979:X) anasema kuwa ndoa ndiyo ukamilisha Mja. Mja hajakamilika bila kuoa au kuolewa. Madai ya Lerner (1979) yanashabihiana na mtazamo wa jamii nyingi za Kiafrika. Lerner (1979) anaendelea kusema kuwa ndoa ni ishara ya mtu kuachana na mambo ya kilimwengu ya anasa. Kwa mtazamo huu basi mwandishi anawaoza Maimuna na Dude ili kuwakamilisha pamoja na kuashiria mabadiliko yao ya kimawazo.

Tafsili nyingine ya ndoa (Engel:1944) ni kuwa, ndoa ni ishara ya ushirikiano na maendeleo. Kutoka jadi hadi wa leo, ushirika unaaminika kama njia mwafaka sana ya kuleta maendeleo katika jamii au katika mtu binafsi. Azima ya mwandishi ya kujenga jamii mpya yeye ushirika inasawiriwa vizuri kupitia kwa ushirikiano wa wanyonge, haswa kupitia kwa ndoa. Ndoa ndiyo taasisi ijengayo msingi wa jamii.

Ijapokuwa Shemsha alizaliwa katika aila ya Kimwinyi, anaonekana ni mtetezi wa wanyonge. Baada ya kumaliza masomo yake ya utabibu, tunaona yungali anamtaka Dude awe mume wake. Dude kijana ambaye hajaona darasa la kwanza. Hoja hii inatudhihirishia kwamba mwandishi anapendekeza jamii ya ushirika isiyo na ubaguzi wa pesa, elimu na kadhalika.

Ndoa ya Shemsha na Dude , Maimuna na Kabi ni zao la mtazamo mpya wa ndoa katika riwaya za Said Ahmed Mohamed. Ndoa zote tunazosawiriwa katika riwaya za Said Ahmed Mohamed zinaonyesha michafuko inayojikita katika vipengee viwili, pesa na uasherati. Hivi vigezo viwili ndivyo hutambulisha ukahaba kama tulivyoelezea katika Sura ya Pili. Katika Asali Chungu, ndoa ya Amina na Zuberi, Pili na Shaabani Supu zilijengeka katika misingi ya kifedha na uasherati. Katika Dunia Mti Mkavu, ndoa ya Fauz na Masika ilivutwa kwa uwezo wa pesa za Bwana Hamound (uk. 21). Ndoa ya Maksuudi na Tamima, Selume na Shoka katika Utengano ni ndoa zilizosheheneza uasherati wa hali ya juu. Mhusika Juba alimhini mke wake wa kwanza mapenzi kwa sababu ya mke wa pili. Maelezo haya ni kwa mujibu wa riwaya ya Kiza Katika Nuru.

Hoja dhahiri ni kuwa ndoa ni taasisi inayoendeleza ukahaba na ukandamizaji. Mwandishi anashtumu ndoa za aina hii. Ndoa za maafa. Ndoa zinazoendeleza maonevu, unyonge, ubinafsi na ukandamizaji. Ni muhimu tufahamu kwamba ndoa hizi ambazo tumezitaja zinatokana na matabaka yote. Hali ya ndoa hizi inaonesha kinagaubaga uoza wa jamii. Uoza wa aina hii ndio umewazaa watu wengi kama Maimuna, Dude, Semeni na wengine katika jamii. Taasisi iliyo muhimu katika jamii ni ndoa. Ndoa ndiyo nguzo ya malezi ya watoto wajengayo jamii. Uoza katika ndoa ni uoza katika malezi ya watoto.

Njia moja ya kusafisha 'uchafu' huu ni kuchukua mwamko mpya wa ndoa katika jamii. Ndoa zisizothamini fedha. Ndoa ambazo ni kielelezo cha mapenzi ya dhati. Wale ambao wameelimishwa na mifumo ya kijamii na kulazimika kutenda kinyume na matakwa ya jamii na utu wao, ndio wako katika mstari wa mbele wa kujenga jamii-mpya. Hawa ambao wameteseka, wamezinduka na wataoana na kuzaa watoto watakaojenga jamii inayoelewa maana ya uhuru, haki, usawa na maendeleo.

Hivyo, kuoa na kuzaa ni taswira inayoonyesha kwamba mapambano ya wanyonge yataendelea. Matatizo

kama waliyoyapata Dude na Maimuna hayatawavunja mioyo wanyonge ambao wako katika harakati za kujikomboa. Tesi za ulimwengu zimempa Maimuna 'kilema'. 'Kilema' kinachowakilishwa na kovu lililoko katika kipaji chake. (Utengano uk. 168). Pia, mumewe, Kabi ana kilema chake kilichotokana na mateso aliyoyapata (uk. 158). Hata hivyo hakuna kukata tamaa maana "penye wimbi ndipo penye njia".

SURA YA TANO

## 5.1. HITIMISHO

Katika uhakiki wetu, tumejishughulisha na suala la ukahaba katika riwaya nne za Said Ahmed Mohamed. Tumenakidi wahusika wanaosawiriwa kama makahaba huku tukitilia mkazo zaidi sababu zinazowaingiza katika ukahaba na namna mwandishi anavyojaribu kuwaondoa kutoka kwa maisha hayo.

Kwa mujibu wa dhana ya ukahaba, tumetumia vigezo vitatu vya kubainisha ukahaba. Kigezo cha kwanza ni faida. Ukahaba huambatana na hali ya kuchuuza mwili kwa matumaini ya kunufaika. Manufaa haya ni kama vile pesa, kazi, mavazi, cheo na faraja nyinginezo. Kulingana na kigezo cha faida, jamii ya makahaba imepanuka na kuvuka madanguro. Hoja ni kwamba kuna namna nyingine nyingi za uhusiano ambapo misingi yake ni kufaidika. Mathalani, uhusiano wa 'Mashuga mami' au 'mashuga dadi' una nguzo za faida. Hivyo basi, hatuna budi kuwahesabu katika jopo la makahaba.

Kigezo cha pili ni idadi ya wateja. Ukahaba mara nyingi huambatanishwa na idadi kubwa ya wateja. Hii ni kwa mujibu wa kutaka

kujinufaisha. Hata hivyo, kigezo hiki si madhubuti kwa kuendeleza vizuri jamii ya makahaba. Hii ni kwa sababu ukahaba una matabaka. Mara nyingi, makahaba wa tabaka la chini wanaopatikana katika madanguro ndio huwa na wateja wengi zaidi. Wale wa tabaka la juu aghalabu hujihusisha na watu fulani wenye hadhi kama vile wanasiasa, wanafalsafa na kadhalika. Uamuzi wetu ni kuwa, idadi ya wateja wa makahaba hutegemea tabaka.

Katika kuendeleza dhana ya ukahaba, tumebainisha kigezo cha ukosefu wa udhati katika 'mapenzi'. Mara nyingi makahaba na wateja wao huwa hawana muumano wa kihisia. Msingi wa uhusiano wa kahaba na mteja ni faida. Kutokana na azima hili, mahusiano yao hayaonyeshi hali ya kustawi maana washiriki huwa na nia ya kuridhisha nafsi zao. Kuridhika kiuchumi pamoja na kuzima moyo wenye tamaa za kimwili.

Tumeelezea dhana ya ukahaba kama uhusiano wa mwanamke na mwanamume wa kushiriki kitendo cha kuonana kimwili kwa matumaini ya pesa au faida nyingine. Uhusiano huu si wa kudumu na mara nyingi hufika kikomo mara tu kitendo kinapokamilika. Wa aidha, wote huridhika kwa hali na mali.

Katika upembuzi wetu wa wahusika makahaba, tumebainisha aina nne za ukahaba. Tumejadili ukahaba unaoendelezwa katika madanguro na vichochoroni. Huu ndio ukahaba duni zaidi. Pia, tumepambanua namna ambavyo wasichana huwajibika kujiuza ndipo wapate kazi au waongezwe mishahara. Licha ya hayo, tumefafanua kipengee cha 'mashuga mami' na 'mashuga dadi' katika kuendeleza ukahaba. Mwisho, tumejadili ukahaba wa tabaka la juu kwa miktadha miwili. Muktadha wa kwanza ni mahali. Kuna wale vipusa ambao huwaburudisha waungwana (watu wa tabaka la juu kiuchumi) katika mahoteli makubwa. Wasichana hawa aghalabu hujipatia wateja wa tabaka la juu katika mahoteli haya. Pia, tumebainisha ukahaba wa tabaka la juu kwa muktadha wa wateja. Kwa muktadha huu, kuna baadhi ya wanawake makahaba ambao hujihusisha na wanaume wenye hadhi na heba.

Suala kubwa na lenye utata ambalo tumekumbana nalo katika tasnifu hii ni suala la kwa nini wanawake na wanaume wengi hujiingiza katika ukahaba. Elimu--jamii huelezea kuwa watu wengi huzama katika ukahaba kutokana na sababu za kiuchumi. Wa aidha, wengine huwajibika kushiriki ukahaba na tabia ya uasherati kama faraja kwa ndoa zisizoridhisha kutokana na

uzee, ugonjwa, kutoelewana na kadhalika. Elimu-nafsia hudai kwamba makahaba ni watu ambao wana kasoro katika kukua kwao. Kwa hivyo Wanaelimu - nafsia huhusisha ukahaba na hali ya kutokomaa kwa nafsi.

Uchanganuzi wa kijamii, kiuchumi na kisaikolojia unadhihirisha kuwa ukahaba ni udhaifu. Makahaba wote huwa na udhaifu wa aina moja ama nyingine. Kuna wale wenye uhitaji mkubwa wa kiuchumi na kuna wengine wenye nafsi ambazo zimelemezwa na na tamaa za kimwili.

Taasisi ya kwanza anayokumbana nayo mtoto anapozaliwa ni familia. Elimu-jamii yasisitiza kwamba ili mtoto abobezwe kikamilifu katika jamii yake na aifae katika utu uzima, ni muhimu kupitia katika familia iliyo na baba na mama. Inaaminika kwamba familia humfunza mtoto jinsi ya kukaa katika jamii na jinsi anavyoweza kuitumikia jamii. Elimu-nafsia yasisitiza kwamba malezi anayopewa mtoto katika familia yake huijenga tabia yake ya baadaye.

Utafiti wetu unadhihirisha kwamba makahaba wengi hutoka katika aila zilizo na kasoro. Mathalani, kufiwa na wazazi, wazazi kwenda utoroni na mara nyingine kupewa malezi yenye kasoro kama vile kutawishwa.

Kutokana na malezi yasiyo na mwelekeo mzuri pamoja na kutengwa na walezi, wasichana na wavulana wengi wamekosa mihimili na maandalizi mazuri ya kukabiliana na ulimwengu. Hali hii imewawezesha wengi kunaswa na hila za kilimwengu na kutumbukia katika ngoma za ukahaba.

Imebainika katika tasnifu hii kwamba wanawake na wasichana wengi makahaba ni wale waliopatwa na mkosi wa talaka na himila bila kuolewa. Talaka na himila bila kuolewa aghalabu husheheneza madhila ya kiuchumi. Kutokana na ukweli kwamba nafasi za kazi ni haba sana katika jamii tunamoishi, ukahaba umetumiwa kama suluhisho la kiuchumi na watu waliopatwa na mikosi mbalimbali katika maisha yao.

Katika kila jamii, watu wamepewa wajibu fulani na jamii zao. Mathalani, kuna wazazi, kuna viongozi wa kisiasa, viongozi wa makanisa na kuna waalimu. Kwa mtazamo wa Kiafrika kila mzee ana wajibu maalum wa kutekeleza katika jamii. Viongozi hawa wanatarajiwa kuiongoza jamii vizuri na wao huwa kama wazazi wa watoto wa jamii zao. kwa mujibu wa tasnifu hii watu wamepuuza wajibu wao. Baadhi ya viongozi hutumia vyeo vyao na uwezo wao wa kifedha kuwapotosha watoto na watu wengine duni. Upotovu huu umewaacha wengi

wakiwa makahaba.

Kuna mshabaha mkubwa kati ya ukahaba na mazingira ya mjini. Maisha ya mjini yamechafuliwa na athari mbaya, za kigeni kama vile uhuru wa mapenzi, uhuru wa wasichana wavulana kushiriki ulevi, pamoja na mapambo ya bei ghali. Sura hizi za maisha ya miji zina uhitaji kubwa sana wa kiuchumi. Ili kushiriki katika maisha haya ghali, watamba -na-njia wengi wamewajibika kujiuza.

Hoja hii ya ukahaba kujitokeza zaidi katika mazingira ya mji kuliko ya mashambani sharti itazamwe sambamba na idadi kubwa ya watu wanaohamia mijini kila siku. Nyanja za kiuchumi katika miji hazijapanuka kiasi cha kutosheleza mahitaji ya mahamia wake. Tena, ni muhimu ifahamike kuwa hawa mahamia sharti washirikishwe katika jamii. Elimu-jamii yadai kwamba ili mtu aweze kukubalika katika kikundi cha watu fulani ni sharti aziige tabia za kikundi hicho. Kwa hivyo, wavulana na wasichana wengi wametumbukia katika ukahaba baada ya kuathiriwa na marafiki.

Kutokana na hali ngumu ya maisha ya mjini, mwandishi anapendekeza watu warejee mashambani maana maisha katika

mazingira haya kwa kiasi fulani ni mazuri na hayajaingiliwa na athari mbaya za kigeni. Athari ambazo zimechangia sana kuwepo kwa ukahaba mijini.

Wa aidha, mwandishi anatutahadharisha dhidi ya kuthamini pesa kuliko utu na miili yetu. Yaani tusiwe watumwa wa pesa. Maisha ya ukahaba ya kuthamini pesa ni adhabu na hayana hadhi yoyote. Kwa hivyo, bora tujiimarishe kupitia kwa ndoa na kilimo ambapo utu wa binadamu utaweza kuthaminiwa. Ni sharti ifahamike kwamba ukahaba unaweza kupungua kama taasisi ya ndoa itachukua mtazamo mpya wa kuthamini haki na usawa.

Baadhi ya makahaba huhiari kifo kuliko maisha. Kwao, maisha ya ukahaba ni adhabu. Adhabu kutokana na hali ngumu ya maisha. Kifo kwa huu muktadha ni silaha ya mwandishi ya kushtumu maangamizi ya jamii. Kwa upande mwingine, kifo kinafikiriwa kuwa suluhisho la maisha ambayo yanaonekana kuwa adhabu. Suluhisho kama hili halitufikishi mbali kwa sababu ni la kukatisha tamaa. Kujiua ni namna moja tu ya kukwepa ukweli wa maisha na wala si njia ya kukabiliana na ugumu wa maisha. Ni afadhali mtu kuyaishi maisha vile yalivyo huku akiwa na matumaini kwamba mwanadamu ana uwezo wa kubadilisha hali yake.

Makahaba wengi hasa wale wa tabaka la chini ni watu ambao wamejaribu njia nyingi za kupata furaha hapa duniani lakini wamekosa. Hivyo, wengi wao ni watu ambao wamekata tamaa na wamejisalimisha kwa tesi zote za ulimwengu.

Ukahaba ni zao la jamii, jamii imezaa makahaba kutokana na ufinyu wa nyanja za uzalishaji mali pamoja na tadi na ubinafsi miongoni mwa wanajamii wenyewe. Kupanuliwa kwa nyanja za uzalishaji mali katika jamii sambamba na utekelezaji wa haki na usawa miongoni mwa wanajamii ndiyo njia ya kipekee inayoweza kupunguza kuwepo kwa ukahaba. Hii ina maana kuwa jamii tunayosawiriwa na Said Ahmed Mohamed inahitaji mabadiliko makubwa ya kiuchumi na maadili ya kijamii. Mabadiliko ambayo yatamuweka kila mtu katika mahali pake mwafaka katika jamii pamoja na kuthamini maisha ya wanyonge walio wengi.

## MAREJELEO

Abdalla, M.S. (1976). Mwana wa yungi hulewa. (East African Publishing House).

Adagala, K. (1981). 'Wanja of the Petals of Blood. A study of the women question and imperialism in Kenya' (Karatasi la Semina lililowasilishwa katika Idara Ya Fasihi, Chuo Kikuu cha Nairobi).

Aluko, T.M. (1970). Chief the Honourable Minister (Heinemann).

Arvon, H. (1973). Marxist Aesthetics. (Cornell University Press).

Balisidya, N. (1975). Shida. (Dar-es-Salaam University Press).

Bakwesegha, C. (1982). Profiles of Urban Prostitution. A case study from Uganda. (Kenya Literature Bureau, Nairobi).

Chacha, C.N. (1985). 'Mazingira ya Mwanamke katika fasihi ya Kiswahili. Mapitio ya Rosa Mistika - E. Kezilahabi. Makala katika MWAMKO Toleo. 3. (Jarida la Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi).

Chesaina, C. (1987). Women in African Drama: Representation and Role. (Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu cha Leeds).

Craig, D. (1975). Marxists on Literature: An Anthology. (Penguin Books).

Cruickshanck, (1958). Albert Camus: The Literature of Revolt. (Oxford University Press, London).

Dirasse L. (1978). The Socio-Economic Position of Women in Addis Ababa. The Case of Prostitution. (Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu Cha Boston).

Durkheim, E. (1957). Suicide: A study in Sociology. (Free Press, New York).

Ekwensi, C. (1954). People of the City. (Dakers Press).

____________ (1961). Jagua Nana. (Hutchin, London).

Engel, F. (1944). The Origin of the Family, State and Private Property. (Pathfinders Press).

Finnegan, F. (1979). Poverty and Prostitution. (Cambridge University Press, Ltd.).

Fischer, E. (1959). The necessity of art and ideology. (Penguin Books).

Freud, S. (1974). Introductory Lectures on Psychoanalysis. (Penguin Books).

Gakwandi, S.A. (1977). The Novel and Contemporary Experience in Africa. (Heinemann, London).

Gibbs, J.P. (1968). Suicide. (Harper and Row Publishers).

Gikandi, S. (1978). The growth of the East African Novel. (Tasnifu ya B.A., Chuo Kikuu Cha Nairobi).

Hough, G. (1966). An Essay on Criticism. (Redwood Press, Ltd.).

Hower, E. (1970). "The Post-Independence Literature (Makala Katika East African Journal Toleo 7. Na. 11, uk. 253).

Jans. I. L. (1969). Personality, Dynamics and Assessment. (New York, Brace and World).

Kamunde, M.E. (1983). Kilio cha Wanyonge katika riwaya za Said Ahmed Mohamed. (Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu Cha Nairobi).

Kaufmann, W. (1976). Existentialism, Religion and Death. (The New American Library Inc.)

Kazungu (1984). Utangulizi wa Kina Cha Maisha - S.A. Mohamed (Longman, Nairobi).

Kezilahabi, E. (1971). Rosa Mistika. (East African Literature Bureau).

______________(1974). Kichwa Maji.
(East African Publishing House).

______________(1975). Dunia Uwanja wa Fujo.
(East African Literature Bureau).

Kiango, S.D. (1982). Jeraha La Moyo.
(Foundation Books Ltd., Nairobi).

Kishtainy, K. (1982). The Prostitute in Progressive Literature.
(Allinson and Busby Ltd., London).

Lerner, L. (1979). Love and Marriage: Literature and its Social Context (Edward Arnold).

Little, K. (1973). African Women in Towns.
(Cambridge University Press).

______________(980). The Sociology of Urban Women's Image in African Literature.
(Macmillan Press Ltd.).

Lowry, R.P. (1974). Social Problems: A Critical Analysis of Theories and Public Policy.
(Health and Company, Canada).

Mailu, D.G. (1974). After 4.30.
(Comb Books: Nairobi).

______________(1976). Unfit for Human Consumption.
(Comb Books: Nairobi).

Mantago, S. (1970). Trial of Jomo Kenyatta
(Secker and Warburg).

Marxist, K. na Engel, F. (1966). Selected Works Vol. I and III. (Political Publishing House, Moscow).

Mazrui, A.M. (1984). 'Mapitio ya Dunia Mti Mkavu' (Makala katika Kiswahili Journal Toleo 51/1 na 51/2.

Mbilinyi, M. (1983). Women in Tanzania: Analytical Bibliography. (Motala Crafisika, Sweden).

McKee, J. (1965). Introduction to Sociology. (New York, Holt Rinehart and Winston Inc.)

Mlacha, S.A.K. (1984) 'Mapitio ya Riwaya za Visiwani (1970-1980) na ujenzi wa jamii mpya' (Makala katika MULIKA Na. 16).

Mkufya, W.E. (1978). The Wicked Walk. (East African Publishing House).

Mohamed, M.S. (1972). KIU. (East African Publishing House).

____________ (1976). Nyota ya Rehema. (Oxford University Press).

Mohamed, S.A. (1977). Asali Chungu. (Shungwaya Publishers Limited, Nairobi).

_______________(1980). 'Sikate tamaa
(Longman, Nairobi).

_______________(1980). Utengano.
(Longman, Nairobi).

_______________(1980). Dunia Mti Mkavu.
(Longman, Nairobi).

_______________ (1983). 'Kupatana na riwaya zangu'
(Makala katika MWAMKO Toleo 2).

_______________ (1984). Kina cha Maisha.
(Longman, Nairobi).

_______________(1988). Kiza katika Nuru.
(Oxford University Press, Nairobi).

Muga, E. (1980). Studies in Prostitution: East, West and South Africa, Zaire and Nevada. (Kenya Literature Bureau, Nairobi).

Mulokozi, M.M. (1982) "Protest and Resistance in Swahili Poetry 1600-1885". (Makala Katika Kiswahili Journal Toleo 49/1).

Musau, P.M. (1987). Euphrase Kezilahabi: Mwandishi aliyekata tamaa. (Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi).

Mutiso, G.C.M. (1971) "Women in African Literature" (Makala katika East African Journal Toleo 8 Na. 3 uk. 4-13.

___________(1974). Socio-political Thought in African Literature. Weusi? (Macmillan).

Mwangi, M. (1976). Going Down River Road. (Heinemann).

_____________ (1978). Kill Me Quick. (Heinemann).

_____________ (1979). The Cockroach Dance. (Heinemann).

Nabhany, S. (Mhariri, 1972). Sanaa ya Utungo I (Heinemann).

Nazarethi, P. (1972). Literature and Society in Modern African. (Kenya Literature Bureau).

_____________ (1978). The third World Writer: His Social Responsibilities. (Kenya Literature Bureau).

Ngara, E. (1982). Stylistic Criticism and The African Novel. (Heinemann).

_____________ (1985). Art and Ideology. (Heinemann).

Ngugi wa Thiong'o (1972). Petals of Blood. (Heinemann, London).

Njogu, S.K. (1987). Maudhui ya Mapinduzi katika riwaya za Visiwani Zanzibar. (Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu Cha Nairobi).

Okello, O. (1963). Prostitute. (East African Publishing House, Nairobi).

Palmer, E. (1979). The growth of the African Novel. (Heinemann, London).

P'Bitek, O. (1966). Song of Lawino. (East African Publishing House, Nairobi).

_____________ (1971). Two Songs. (East African Publishings House, Nairobi).

Peck, J. na Coyle, M. (1984). How to study Literature, Literary terms and criticisms. (Macmillan Limited).

Pickvance, G.C. (1976). Urban Sociology: Critical Essays. (Tavistock Publication, London).

Raymond, W. (1975). The country and the City. (Paladin, London).

Reed, E. (1970). Problems of Women's Liberation. (Pathfinder Press).

Robey, D. na Jefferson N. (Wahariri, 1982): Modern literary Theory: A Comparative Introduction. (Batsford Academic and Educational Limited, London).

Senkoro, F.E.M.K. (1982). The Prostitute in African Literature. (Tanzania Publishing House, Dar es Salaam).

Singh, J. (1965). Sweet Schum of Freedom (Heinemann).

Slaughter, E. (1980). Marxism, Ideology and Literature. (Macmillan Press Limited).

Smart, C. (1976). Women, Crime and Criminology. (Routledge and Kegan Paul).

Strobel, M.N. (1975). Muslim Women in Mombasa, Kenya 1966-1973. (Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu Cha California, Los Angeles).

Teyie, J.A.O. (1982). Meja Mwangi: The Urbanization of a Writer: An Analysis of Kill Me Quick, Going Down River Road and The Cockroach Dance. (Tasnifu ya B.A., Chuo Kikuu Cha Nairobi).

____________ (1986). Indiviualism in the East African Urban Novel. (Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu Cha Nairobi).

Vigor, P.H. (1966). A guide to Marxism and Its Effect on Soviet Development. (Humanities Press).

Welleck, R. na Warren, A. (1949). Theory of Literature (Penguin Books).

White, M.A. (1977). Socialization. (Longman, New York).

Worsely, P. 1970). Introducing Sociology.
(2nd Edition). (Penguin Books).

Zola, E. (19 ? ). Nana.
(Garden City, New York).

UNIVERSITY LIBRARY